SportPesa
TZS. 918,137,180
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 3

**KISWAHILI** rasmi kutumika vikao AU




UKURASA 11

# Nipashe

Jumanne Februari 8, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580850

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

**KES I YA MBOWE**

## Askari: Hatukushuhudia akipanga kufanya ugaidi

UKURASA 2



UKURASA WA 4

### KIJANA ADAIWA KUUA KAKA YAKE KWA KISU

MKAZI wa Mtaa wa Burka, Kata ya Olasiti mkoani Arusha, James Sindiu (16)...

UKURASA WA 7

### KAMPENI YA MLANGONI TRA YAIBUA W'BIASHARA

FEBRUARI mosi, 2022 serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)...

UKURASA WA 8

### SHERIA MPYA UTAKATISHAJI WA FEDHA YAPENDEKEZWA

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimependekeza kutungwa upya..



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na wananchi wa Butiama mkoani Mara wakati akielekea wilayani Bunda, jana. **PICHA: IKULU**

## Wasira: Samia anatosha 2025

**RAIS** aagiza wakaguzi wa ndani kuhamishwa...*Endelea ukurasa 2*

**HATI FUNGANI**




Ofisa Mtendaji Mkuu Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, akizindua hati fungani maalum 'NMB Jasiri Bond' jijini Dar es Salaam jana, huku maofisa wa ngazi za juu wa benki hiyo wakishuhudia. **Habari Uk. 7. PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Polisi wa Mtwara kortini tena leo

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA YATAJA SABABU KUKOSA MABAO LIGI KUU UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza wakati akiongoza kikao cha Kamati Kuu ya Taifa ya Sensa, kwenye ukumbi wa Hazina jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Askari: Hatukumshuhudia Mbowe akipanga ugaidi

**Na Kulwa Mzee**

INSPEKTA Tumaini Swila amedai yeye pamoja na wapelelezi wenzake hawakuwahi kumshuhudia Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe akiwa katika kikao cha kupanga njama za kufanya vitendo vya kigaidi.

Swila ambaye ni shahidi wa 13 wa Jamhuri alidai hayo jana Mahakama Kuu, Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joackim Tiganga wakati akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Nashon Nkungu.

Alidai kupitia ushahidi aliotoa anaweza kusimama kifua mbele kwamba alitenda haki katika kufanya uchunguzi wa kesi hiyo.

Anadai katika kufanya kazi zao za upelelezi waliongozwa na Sheria ya Kuzuia Ugaidi na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

Inspekta Swila anadai yeye pamoja na wapelelezi wenzake hawakuwahi kumshuhudia Mbowe akiwa katika kikao cha kupanga kufanya ugaidi.

Anadai hawakuwahi kumshuhudia Mbowe akiwa katika kikao cha kupanga kufanya ugaidi Mkoa wa Mbeya au Arusha kama ambavyo inadaiwa katika hati ya mashtaka kuwa walikula njama katika mikoa mbalimbali ikiwamo mikoa hiyo.

Shahidi anadai wapelelezi hawana CCTV camera wala sauti ya Mbowe wakati akipanga kufanya ugaidi.

Akiendelea kuhojiwa na Wakili Nashon, alidai msiri wao katika kesi hiyo alikuwa Luteni Dennis Urio na katika kushiriki kufanya upelelezi hakuwahi kufika Aishi Hoteli.

Awali akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando, shahidi alidai allipokea taarifa za uchunguzi na silaha ambayo ni bastola aina ya Luger A5340, risasi moja na vichwa viwili vya risasi.

Anadai alipokea taarifa hiyo kutoka kitengo cha uchunguzi wa silaha na milipuko, risasi aliyopokea moja ilikuwa haijatumika, vyote alivyopokea alikabidhi kwa Sajenti Nuru Kituo cha Polisi cha Kati Dar es Salaam.

Machi 30, mwaka 2020, anadai alipokea taarifa ya maabara ya kisayansi kutoka kitengo cha uchunguzi, ripoti ilionyesha sampuli za maandishi yaliyochukuliwa kutoka kwa mshtakiwa Halfani Bwire ni sawa na maandishi yaliyokuwapo katika kidaftari kidogo.

Anadai kidaftari hicho kina michoro ya ramani za vituo vya mafuta, majina ya barabara, mishale ya kuingia na kutoka, pia walitaja kituo cha mafuta cha BP na Bigbon.

Akihojiwa na Wakili wa Utetezi, John Mallya, shahidi anadai wakati anakabidhiwa simu na Luteni Dennis Urio alikutwa ofisi ndogo ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Dar es Salaam.

Alipohojiwa aseme kama kumtukana Rais kwenye mtandao ni kuhatarisha usalama wa nchi ndio au hapana, shahidi alidai hapana lakini ugaidi ni kuhatarisha usalama wa nchi.

Anadai maelezo ya Justine Kaaya yalichukuliwa Julai 30, mwaka 2021, kuhusu tuhuma za ugaidi wakati washtakiwa wakiwa wameshakamatwa.

Shahidi alikiri anayo taarifa kuwa mwaka huu masoko yameungua moto Moshi na kwingineko.

Inspekta Swila anadai ni uongo kwamba kuungua moto kwa masoko ni sababu ya laana ya kumsingizia Mbowe kesi ya ugaidi.

"Hilo ni kosa moja, lakini washtakiwa kwa makosa mengine ya kukata miti barabarani, kupanga njama za ugaidi na kutaka kuwadhuru viongozi wa serikali," alidai.

Anadai wakati anaandika taarifa ya kwenda maabara ya kisayansi simu ya Kaaya na wenzake alikuwa nazo na kwamba Mbowe na Kaaya waliwasiliana wakati washtakiwa wengine wakiwa wameshakamatwa.

Shahidi anadai line za simu za Luteni Urio ziko kwenye simu zake zilizoko mahakamani kama kielelezo.

Wakili Mallya alidai Jaji apime ukweli uliko kwa sababu simu za Luteni Urio hazina line.

Shahidi anadai kwamba malalamiko yalianzia kwa DCI, lakini Afande Ramadhan Kingai alimwelekeza akafungue jalada la kesi Kituo cha Polisi cha Kati Dar es Salaam.

Anadai Afande Kingai hakumweleza kwanini asifungue jalada hilo Kituo cha Polisi Temeke au Oysterbay.

# Wasira: Samia anatosha 2025

**Na Jenifer Gilla**

MWANASIASA mkongwe nchini, Stephen Wasira, amesema Rais Samia aachwe amalizie vipindi viwili vya urais kama ilivyo utamaduni wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Aliyasema hayo jana mkoani Mara alipopewa nafasi ya kuzungumza baada ya Rais Samia kuweka jiwe la msingi katika ujenzi wa chujio la maji wilayani Bunda.

"Wale waliosema wanataka urais 2025, mimi nawashauri wasubiri kwa sababu kwa utamaduni wa CCM kama kuna rais aliyepo ofisini huwa hatumpingi, tunampa nafasi amalizie awamu hiyo ambayo ni miaka 10," alisema Wasira.

Alitoa mfano wake binafsi kwamba aliwania urais, lakini hakuupata na sasa kwa kuwa ameshapitwa na umri, amekaa pembeni na hana nia tena ya kuwania.

Wasira aliwataka wenye dhamira hiyo ya urais wasubiri hadi vipindi viwili vya Rais Samia vipite, na iwapo watakuwa wamepitwa na umri waige mfano wake, ambaye amejiunga na wazee wa Mara maana si wote lazima kuwa rais bali ni fursa ya mtu mmoja.

Akiongelea mradi wa maji alimpongeza Rais kwa kuwapatia fedha za mradi huo ulioasisiwa mwaka 1974 na hatua ya jana ndio inakamilisha ujenzi wa mradi huo.

Pia alimshukuru Rais kwa kuwapatia fedha za miradi mingine ya maendeleo ikiwamo kujengea shule, hospitali na maji katika mkoa huo.

SAMIA AWASHUKIA WAKAGUZI

Rais Samia Suluhu ameagiza wakaguzi wa ndani katika mkoa wa Mara wabadilishwe vituo vyao kutokana na ufujaji wa fedha za miradi ya maendeleo zinazotolewa na serikali hali inayosababisha utekelezaji wa miradi mkoani humo kuchelewa. Pia aliiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani humo kuhakikisha wanafuatilia kupambana ili kudhibiti matukio ya ufujaji wa fedha yanayoendelea ndani ya halmashauri.

Rais aliyasema hayo jana baada ya kuweka jiwe la msingi katika ujenzi wa chujio la maji katika mradi wa maji Wilaya ya Bunda.

"Bado ndani ya mkoa miradi kadhaa pesa zinafujwa, pesa zinaliwa na hakuna ripoti unayopata mpaka mwisho wa mwaka ndio mkaguzi anasema halmashauri hii haikufanya vizuri … madudu haya hayaonekani mapema kwa sababu wakaguzi wa ndani ni sehemu ya wafujaji wa fedha hizo, ndio maana hamkagui wala hamsemi," alisema Rais na kuongeza:

"Kwa hiyo Waziri wa TAMISEMI, sijui hawa ni wa kwako, au wa Waziri wa Fedha? Waziri yeyote ambaye anashughulikia hawa watu, basi wabadilisheni, wamekaa sana wamezoeana, wabadilisheni waweze kufanya kazi yao," alisema Rais.

"Mimi naomba mfanye kazi yenu wakati miradi imeingia, mnafuata hatua kwa hatua, kupambana , kuzuia vitendo vya rushwa, ndio kazi yenu, lakini mpo huku mmestarehe mnasubiri ripoti za mkaguzi wa mahesabu ndio mnaanza sasa kufukuzana kwenda kuwadhibiti wale waliofanya makosa," aliagiza Rais.

Alisema sababu nyingine ya ucheleshwaji wa miradi ya maendeleo ni uzembe na mivutano ndani ya mkoa na kuhusu wapi fedha za miradi zielekezwe pale zinapotolewa na serikali.

"Utekelezaji wa miradi ndani ya mkoa unachelewa sana, moja ni kwa sababu ya uzembe, lakini kuna ufujaji wa fedha, lakini tatu kuna mivutano ndani ya mkoa huu, mivutano ya mradi uende wapi, mwingine anavutia kwake kwa ubinafsi tu bila kujua kuwa upande uliotarajiwa huduma ziende ni wenye wananchi wengi," alisema.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mara, Samuele Kiboye , maarufu Namba Tatu alimwambia Rais Samia kuwa katika mkoa huo kuna madiwani wanachukua tenda za halmashauri kwa manufaa yao binafsi kinyume na sheria.

"Sheria inakataza madiwani kuchukua tenda ya halmashauri, lakini Mheshimiwa Rais kuna madiwani wanachukua fedha, na hizo halmashauri nitakuja nikwambie…mheshimiwa Rais nitakuletea majina yao," alisema.

HABARI KITAIFA

# Polisi wanaotuhumiwa mauaji kortini tena leo

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

KESI ya tuhuma za mauaji ya mfanyabiashara wa madini, Musa Hamis (25), mkazi wa Kijiji cha Ruponda Wilaya ya Nachingwea Mkoa wa Lindi, inayowakabili maofisa saba wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mtwara inatarajiwa kuendelea leo, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Mtwara.

Watuhumiwa hao watapandishwa kortini mara ya pili kwa ajili ya kutajwa.

Maofisa wanaotuhumiwa katika mauaji hayo ni Mrakibu wa Polisi, Gilbert Kalanje, aliyekuwa Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Mtwara (OC- CID), Mrakibu Msaidizi wa Polisi, Charles Onyango, aliyekuwa Mkuu wa Kituo cha Polisi Mtwara (OCS), Mrakibu wa Polisi Msaidizi Nicholaus Kisinza.

Wengine ni Mkuu wa Intelijensia ya Jinai Mkoa wa Mtwara, Mkaguzi wa Polisi John Msuya, Mganga Mkuu Zahanati ya Polisi Mtwara, Mkaguzi wa Polisi Msaidizi Marco Mbuta, Mkaguzi wa Polisi Shirazi Mkupa na Koplo Salimu Juma Mbalu.

Januari 5, mwaka huu, watuhumiwa hao wanatajwa kula njama na kisha kumuua mfanyabiashara wa madini, Musa Hamis kisha kuutupa mwili wake katika Kijiji cha Hiari Wilaya ya Mtwara.

Mara ya kwanza watuhumiwa hao walifikishwa mahakamani Januari 15, mwaka huu, baada ya kukamatwa na kuhojiwa katika vituo mbalimbali vya polisi kati ya Januari 22 na 24.

Musa anadaiwa kukumbana na kadhia hiyo ya mauaji wakati akidai fedha zaidi ya Sh. milioni 33.7 zilizochukuliwa na maofisa hao baada ya kumkamata Oktoba 20, mwaka huu, akiwa katika nyumba ya kulala wageni ya Sadina iliyoko mkoani Mtwara.

Kwa Mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Mark Njera, wakati huo Musa alionekana akifanya matumizi yasiyo ya kawaida na alipokamatwa na kupekuliwa alikutwa na Sh. milioni 2.43 huku akieleza fedha zingine aliziacha nyumbani Nachingwea.

Njera alisema wakati huo askari wake walipofika katika Kijiji cha Ruponda, walifanikiwa kukuta Dola za Marekani 13,558 na kufanya jumla ya fedha zote kuwa Sh. milioni 33.7.

# Kiswahili sasa rasmi kutumika vikaoni AU

**Na Maulid Mmbaga**

MKUTANO wa 35 wa viongozi wa Umoja wa Afrika (AU) umeridhia na kupitisha ombi la Tanzania kutaka Kiswahili kuwa lugha ya kazi katika vikao vya umoja huo.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango aliwasilisha ombi hilo jana la lugha ya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha za kazi katika kikao cha viongozi wa AU kilichoanza wiki iliyopita mjini Addis Ababa nchini Ethiopia.

Akihutubia katika kikao hicho, Dk. Mpango alisema Kiswahili ni miongoni mwa lugha zenye wazungumzaji wengi barani Afrika na alibainisha kuwa zaidi ya watu milioni 100 wanatumia lugha hiyo pamoja na wazungumzaji wengine kutoka nje ya Bara la Afrika.

Dk. Mpango alisema lugha ya Kiswahili pia tayari inatumika sehemu mbalimbali ikiwamo Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), pamoja na kufundishwa shuleni katika nchi nyingi Afrika.

"Tayari Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni limetangaza Julai saba ya kila mwaka kuwa ni siku ya maadhimisho ya lugha ya Kiswahili duniani," alisema Dk. Mpango.

Aidha, katika upande mwingine mkutano huo pia umeichagua Tanzania kuwa mjumbe wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika.

Pia mkutano huo ulilaani vitendo vya uvunjaji wa katiba vilivyosababisha mapinduzi ya kijeshi katika mataifa mbalimbali, pamoja na vitendo vya ugaidi vinavyoendelea katika baadhi ya mataifa barani Afrika.

Umoja wa Afrika pia ulitoa wito ukisisitiza kuendelea kwa majadiliano katika nchi husika, ili kurejesha utawala wa kiraia na wa kidemokrasia kwa mujibu wa katiba.

AU pia ilitoa wito kwa nchi wanachama kushirikiana katika kukabiliana na janga la UVIKO - 19 ikiwa ni pamoja na kuhakikisha chanjo zinapatikana na kuyaunga mkono mataifa yalioanza jitihada za kuzalisha chanjo hiyo barani Afrika, ikiwamo Afrika Kusini, Senegal na Rwanda.

**Akihutubia katika kikao hicho, Dk. Mpango alisema Kiswahili ni miongoni mwa lugha zenye wazungumzaji wengi barani Afrika na alibainisha kuwa zaidi ya watu milioni 100 wanatumia lugha hiyo pamoja na wazungumzaji wengine kutoka nje ya Bara la Afrika.**




# Dk. Mwinyi aitaka mahakama kusimamia haki za wananchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameitaka mahakama na taasisi zinazosimamia haki kuwa mfano mwema kwa jamii katika kusimamia haki za wananchi.

Aliyasema hayo jana katika maadhimisho ya Siku ya Sheria Zanzibar yaliyofanyika katika ukumbi wa Shekhe Idrisa Abdulwakil Kikwajuni Mjini Zanzibar ambapo kauli mbiu ya maadhimisho hayo ni 'usimamizi wa haki ni msingi wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii'.

Alisema ili kufikia maendeleo ya kweli ya kijamii na kiuchumi, mahakama na tassisi zote za kisheria lazima zibadilike na kuwa karibu na rafiki kwa wananchi.

Alisema lazima kujenga mifumo itakayohakikisha usikilizaji haraka wa mashauri mahakamani pamoja na taasisi zingine za utoaji wa haki.

Dk. Mwinyi alisema kesi zinapomalizika mahakama, zihakikishe wahusika wanapata mienendo ya kesi kwa haraka ili kuwapa fursa ya kukata rufani kwa wakati katika mahakama za juu wale ambao hawakuridhika na uamuzi.

"Haipendezi hata kidogo kuona kwamba wananchi na wawekezaji wetu wanachukua muda mrefu mahakamani na katika taasisi zingine kufuatilia haki zao, kwani wangeweza kutumia muda huo kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo," alisema.

Alieleza malalamiko mengi yanayowasilishwa kwake kupitia mtandao wa 'sema na Rais', yanahusu ucheleweshaji wa utoaji wa haki unaofanywa na baadhi ya viongozi wa taasisi za serikali.

Aliwasisitiza viongozi kuongeza bidii katika kusimamia utoaji wa haki za wananchi kwa kuzingatia sheria na maelekezo ya taasisi zinazosimamia sheria.

Alieleza kuwa usimamizi bora wa haki huambatana na maadili bora kwa watendaji wa sekta za sheria ikiwamo mahakama na nilazima kupiga vita rushwa na vitendo vyote vya kifisadi.

"Wito wangu kwa taasisi zote za haki kuwa mifano bora kwa jamii katika kusimamia haki za watu na kwa sasa hatutarajii haki kucheleweshwa kutokana na miundombinu ya kisasa tuliyojenga na tunayoendelea kujenga," alisisitiza Dk. Mwinyi.

Naye Kaimu Jaji Mkuu wa Mahakama Kuu Zanzibar, Khamis Abdallah Ramadhan, alisema licha ya Rais kupokea malalamiko mengi ya ucheleweshaji wa haki kupitia mtandao wa sema na rais, lakini hajawahi kuingilia muhimili wa mahakama na badala yake ameacha malalamiko hayo yashughulikiwe kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi.

Alieleza kuwa jukumu la msingi la mahakama ni kupokea, kusikiliza na kuyatolea uamuzi mashauri mbalimbali ya jinai na madai yanayofikishwa mahakamani na kwa mwaka 2020/20221 mahakama ilipokea kesi za jinai 8,744 na zilizotolewa uamuzi ni 6,734 na kesi 2,010 zimebaki mahakamani.

Kwa kesi za madai zilizofunguliwa, alisema ni kesi 2568 zilifunguliwa mahakamani na zilizotolewa uamuzi ni 1,484 na mashauri yaliobaki mahakamani ni 184.

Alisema bado kuna changamoto ya mashahidi kutofika mahakamani hasa kwa kesi za udhalilishaji na dawa za kulevya.

Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Dk. Mwinyi Talib, alisema ili kuwa na sheria bora, ofisi yake katika mwaka mmoja uliopita imesimamia na kuzifanyia marekebisho ya sheria mbalimbali ambazo zimesaidia maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Alisema miongoni mwa marekebisho ya sheria hizo marekebisho ya sheria ya ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi sheria namba nane ya mwaka 2015, ambayo ndio inayoongozwa ya kuwekwa misingi ya upatikanaji wa miradi ya uwekezaji.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kushoto), akiagana na Kaimu Jaji Mkuu wa Zanzibar, Jaji Khamis Ramadhan Abdalla Shaaban (katikati), Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, Idrissa Kitwana Mustafa na Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Jaji Mustapha Siyani (kulia) baada ya kutoa hotuba katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Sheria Zanzibar yaliyofanyika jana. **PICHA: IKULU**

# Hatua 6 kukabili ongezeko bei ya vifaa ujenzi, vinywaji baridi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetaja hatua sita inazozichukua kudhibiti ongezeko holela la bei za bidhaa za ujenzi na vinywaji baridi ikiwamo kuwaagiza wazalishaji, wasambazaji na wafanyabiashara kushusha mara moja bei za bidhaa hizo na kuuza kwa kuzingatia gharama halisi za uzalishaji na usambazaji.

Hatua hizo zimekuja baada ya serikali kufanya uchunguzi kupitia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Tume ya Ushindani (FCC) katika kipindi cha Novemba 2021 hadi Februari 2022, ambapo yalibainika masuala mbalimbali ikiwamo ucheleweshaji wa makusudi wa saruji kutoka viwandani.

Akitoa tathmini ya mwenendo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa hizo, Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Ashatu Kijaji, alisema hatua nyingine ni kuziagiza mamlaka zote za udhibiti kuchukua hatua kali dhidi ya walimbikizaji na wauzaji kupitia mlango wa nyuma wanaosababisha bei za bidhaa kupanda sokoni, ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinafika sokoni kwa wakati na kwa bei shindani.

"Kwa kuwa kitendo cha kupanga bei kati ya washindani ni uhujumu uchumi, ninazielekeza mamlaka husika kuchukua hatua kali dhidi ya wote watakaobainika kupanga bei kwa bidhaa kwa mujibu wa sheria za nchi, ninawaelekeza wazalishaji kuzalisha bidhaa hizo kulingana na uwezo wa viwanda uliosimikwa ili kukidhi mahitaji ya soko, ninawaelekeza wazalishaji wa vifaa vya ujenzi kuweka mifumo mizuri ya usambazaji wa vifaa hivyo ili kuzuia kupanda kwa bei kunakoweza kuzuilika," alisema.

Aliwaagiza maofisa biashara wa mikoa nchini waendelee kufuatilia kwa karibu mwenendo wa bei za bidhaa mbalimbali kwenye maeneo yao na kuwasilisha taarifa hizo mara kwa mara wizarani kupitia Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa, ili hatua stahiki zichukuliwe kwa wakati.

Awali, Dk. Kijaji alitaja mambo matano yaliyobainika katika tathmini hiyo kuwa ni ongezeko holela la bei za vifaa vya ujenzi, hususan saruji na nondo linasababishwa na wazalishaji wa bidhaa husika kufanya uzalishaji banifu na kutokuwa na mfumo wa wazi wa usambazaji kutokana na kuwa na mnyororo mrefu wa usambazaji wa bidhaa kutoka kiwandani mpaka kumfikia mlaji wa mwisho. Pia alisema walibaini gharama halisi za uzalishaji wa saruji haiakisiwi katika bei ya saruji iliyoko sokoni ikilinganishwa na uwiano huo katika nchi jirani, ongezeko la bei ya saruji na nondo halina uwiano halisi na gharama za usafirishaji na usambazaji, bei ya saruji iliyoko sokoni haina uhusiano na mwenendo wa nguvu za utashi wa mlaji na ugavi na kuna ucheleweshwaji wa makusudi wa utoaji wa saruji kutoka viwandani kwenda kwa wasambazaji na wanunuzi wa ndani.

Alisema serikali haitavumilia tabia ya wafanyabiashara wachache kuanzia wazalishaji hadi wasambazaji wenye dhamira ovu ya kuwaumiza wananchi kwa kujiamulia kupandisha bei za bidhaa bila kufuata utaratibu kwa manufaa yao binafsi.

## Kijana adaiwa kuua kaka yake kwa kisu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKAZI wa Mtaa wa Burka, Kata ya Olasiti mkoani Arusha, James Sindiu (16) anadaiwa kumuua kaka yake Zakayo Sindiu (24), kwa kumchoma na kitu chenye ncha kali sehemu ya moyo.

Nipashe lilimtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, na kueleza kwamba Jeshi la Polisi bado linamsaka mtuhumiwa huyo.

Akizungumza na waandishi wa habari nyumbani kwake, baba wa marehemu, Paulo Sindui, alisema amesikitishwa na kifo hicho ambacho kilitokea mbele yake Februari 5, mwaka huu.

Sindiu ambaye ni mfugaji wilayani Simanjiro mkoani Manyara, alidai chanzo cha ugomvi huo ni Zakayo kukataa kurudisha mifugo wilayani Simanjiro, kwamba awali ililetwa mkoani Arusha kwa ajili ya malisho kutokana na ukame uliokuwa umekithiri wilayani humo.

"Mimi ni mfugaji, mifugo yangu niliileta huku Arusha kutokana na ukame uliokuwa umekithiri wilayani Simanjiro. Lakini nilipigiwa simu mvua imenyesha hivyo kijana wangu Zakayo, akawa anamwambia mwenzake apeleke mifugo Simanjiro akachunge na yeye akawa hataki," alidai.

Alisema siku ya tukio Zakayo pamoja na mdogo wake James walikuwa nyumbani, ndipo Zakayo akamwagiza mdogo wake James, kurudisha mifugo Simanjiro kwa sababu mvua zimeanza kunyesha, lakini James alikaidi ndipo wakaanza kugombana mbele yake.

Alisema baada ya kuona ugomvi umekuwa mkubwa aliinyanyuka kwa ajili ya kuamua, lakini ghafla James alichomoa kisu na kumchoma kaka yake kwenye moyo na kuanguka chini.

"Baada ya kuona ugomvi unazidi niliamua kusimama kwenda kuwaamu, lakini kutokana na ulemavu wangu wa mguu sikuweza kutembea haraka na wakati nawafikia James akawa ameshamchoma kisu kaka yake," alisema Sindiu.

Sindiu alisema sababu kubwa ya Zakayo kukataa kwenda Simanjiro kupeleka mifugo ni kutokana na maisha ya mjini ambayo alikuwa ameyazoea ya kula maandazi na chipsi, kuangalia runinga tofauti na kule machungani ambapo chakula kikuu ni maziwa.

Alisema kutokana na hali hiyo ndugu waliokuwa nyumbani hapo walianza kupiga kelele za kuomba msaada kisha kumchukua marehemu na kumkimbiza katika Hosptali ya Rufani ya Mount Meru.

Sindiu alisema, "Baada ya kufika hospitalini hapo madaktari waliokuwa zamu walimpokea mwanangu na walipomwangalia walibaini kwamba amefariki na kutupa taratibu za kuhifadhi mwili huo katika chumba cha kuhifadhia maiti."

Sindiu alisema anatarajia kumzika mwanawe Februari 10, mwaka huu nyumbani kwake eneo la Burka jijini Arusha.

HABARI KITAIFA

# Miti milioni 276 kupandwa nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA



WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amesema miti milioni 276 itapandwa mwaka huu nchini na kuwahimiza kutumia mvua zinazoendelea kunyesha kwa kupanda miti ili kufikia lengo hilo.

Waziri Jafo alitoa kauli hiyo jana jijini hapa alipokuwa akiongoza upandaji miti katika eneo la Medeli ikiwa ni sehemu ya Wiki ya Uzinduzi wa Sera ya Mpya ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 ambayo inatarajiwa kuzinduliwa Februari 12, mwaka huu na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Alisema kila halmashauri itapaswa kupanda miti milioni 1.5 na kuwataka viongozi wa maeneo hayo kusimamia ili kufikia lengo hilo.

Pia aliwataka wanafunzi kuendeleza kampeni ya 'Soma na Mti' aliyoizindua hivi karibuni yenye lengo la kupanda miti zaidi ya milioni 14.

"Kwa wale wanafunzi ambao hawajapanda miti kila mwanafunzi Tanzania hii aende kupanda mti wake, tutumie mvua hizi, hongereni wanafunzi mmejitokeza kufanikisha suala hili ili kuifanya Dodoma inakuwa ya kijani," alisema.

Aliwakumbusha wadau wote kushirikiana katika kuibeba ajenda ya upandaji na utunzaji wa miti ili kuondokana na tatizo la ukame lililojitokeza kwa baadhi ya maeneo.

"Pia kila familia tuna lile jukumu la kupanda miti ili kuitendea haki Tanzania yetu, tufanyie kazi ajenda ya mazingira sababu maji yalipungua kwenye vyanzo vingi vya mabwawa sababu ya mabadiliko ya tabia nchi," alisema.

Alisema ajenda ya mazingira itasaidia kuimarisha uchumi wa nchi ili kuitendea haki Tanzania.

Shughuli nyingine zitakazotekelezwa katika wiki hiyo ni upandaji wa miti katika eneo la Iyumbu, Isern, maeneo ya barabara inayoanzia Chimwaga na Chuo Kikuu cha Dodoma kuelekea barabara ya Dodoma - Dar es Salaam.

Aidha, usafi utafanyika pembezoni mwa barabara inayoanzia Shule ya Martine Luther hadi wajenzi kupitia Nzughuni, Ilazo, Ipagala na Area C, kutoa elimu kuhusu utenganishaji wa taka, kufanya usafi katika Soko la Chang'ombe na utoaji wa elimu ya mazingira kwa wananchi na wadau kupitia vyombo vya habari.


halotel

**TAARIFA KWA UMMA**

Viettel Tanzania PLC (Halotel) ni kampuni ya mawasiliano inayoendelea kuboresha huduma na kuvunja mipaka ya mawasiliano kwa wateja wetu kwa kutoa gharama nafuu kwenye SMS, Huduma za kupiga simu na Intaneti.

Tunapenda kuwatangazia wateja wetu na umma kwa ujumla juu ya gharama za makato nje ya kifurushi.

**GHARAMA ZA KUPIGA NCHINI**

| Piga kwenda mitandao | Gharama (Tsh/Dk) |
|---|---|
| Halotel - Halotel | 30 |
| Halotel - mitandao mingine | 30 |

**GHARAMA KUPIGA ZA NJE YA NCHI**

| Kanda | Gharama (Tsh/Dk) |
|---|---|
| **Ukanda 1:** USA, UK, India, China, Canada, Australia, Japan, South Korea, Vietnam, Laos, Cambodia | 450 |
| **Ukanda 2:** Nchi nyingine za ULAYA, Kenya | 750 |
| **Ukanda 3:** Rwanda, Afrika Kusini, Zambia, UAE, Oman,Haiti, Peru | 840 |
| **Ukanda 4:** Cameroon, Zimbabwe, Malawi, Uganda, Congo DRC, Mozambique | 1,000 |
| **Ukanda 5:** Burundi | 1,350 |
| **Ukanda 6:** Sehemu nyingine duniani | 2,700 |
| **Ukanda 7:** Mitandao ya satelite | 13,800 |

**GHARAMA ZA SMS**

| SMS | Gharama |
|---|---|
| SMS ndani ya nchi | 5 Tsh/SMS |
| SMS kimataifa | 95 Tsh/SMS |

**GHARAMA ZA INTANETI**

| Data (MBs) | Gharama |
|---|---|
| MB | 7.5 Tsh/MB |

166944 Halotel Tanzania Hotline 100



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONYESHA NIA: HUDUMA ZA KUSANIFU NA KUKARABATI OFISI**
**KUMBUKUMBU NAMBA. 0010007463**

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inaalika taasisi (kampuni) zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kusanifu na kukarabati ofisi kwa ajili ya Maradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, MkoawaTanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

Kwa minajiri ya Kujenga uwepo wetu jijini Dar Es Salaam, Kampuni ya EACOP itakuwa inawakaribisha wafanyakazi na wazabuni zaidi ya 300 katika mwaka ujao. Ili kupata ofisi katika wiki zijazo, EACOP inatarajia kuchagua mzabuni atakayesaidia kusanifu na kukarabati eneo la ofisi hiyo kulingana na mahitaji ya kampuni yetu inayokua.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

- Kusanifu, kujenga na kupangilia ukarabati ndani ya eneo lililotengwa.
- Kupata vifaa ndani ya muda kadri inavyohitajika.
- Usanifu na ujenzi wa ndani.
- Upangaji wa nafas iza kukaa.
- Uwezo wa kusimamia kazi husika.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni/Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Rekodi inayoonyesha uzoefu wa kutosha katika kusanifu, kujenga na kukarabati ofisi ndani ya jiji la Dar es Salaam kwa kipindi kisichopungua miaka kumi.
- Iwe na uwezo wa kusanifu na kurekebisha michoro na ramani inavyostahili kulingana na huduma zilizopo kwenye zabuni.
- Ionyeshe uwezo wa kufanya kazi ndani ya ratiba na bajeti ya Mradi.
- Uwezo wa usimamizi wa Afya Usalama na Mazingira uliothibitishwa kwa shughuli za ukarabati wa ofisi.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Inashauriwa kuwasilisha maombi ya usajili kwenye kazi data ya EWURA ya Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) wakati wa konesha katika maombi haya.
- Kuzingatia kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani.
- Leseni ya biashara inayodhibitisha kufanya kazi hii.

Kampuni zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya saa **11** alasiri saa za Afrika Mashariki (EAT), tarehe **21 Februari 2022 .** Kichwa cha Barua pepe kiwe **0010007463.**

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya (Makampuni) ya awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko wa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa taasisi za awali zenye vigezo baada ya taasisi hizo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA). Maombi yote ya kuonesha nia ni lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.

166939

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maoni ya wadau sheria ya ugaidi yazingatiwe

**JUMAMOSI** Bunge lilikaribisha wadau mbalimbali kutoa maoni kwenye muswada wa Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu, ambao ndani yake una vifungu vya taratibu za waziri kutunga kanuni za kumtangaza mtu kuwa gaidi wa ndani.

Aidha, sheria hiyo imeainisha mambo ambayo yatahesabika ni ugaidi kuwa ni kusababisha hofu, vitisho na maandamano ambayo yatasababisha kifo au vifo basi mhusika atashtakiwa kwa ugaidi.

Licha ya wadau kuitwa kutoa maoni yao waliojitokeza mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, waliofika Jumamosi ni Kituo Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), jambo linalozua maswali kuwa wadau wengine wako wapi na kwanini hawakuja mbele ya kamati kutoa maoni yao.

Ni kawaida watu wanaitwa kutoa maoni hawajitokezi au wanajitokeza wachache, sheria inapopitishwa ndipo malalamiko hujitokeza kwa wingi kuwa ni mbovu au haikujali maslahi ya umma.

Wanapojitokeza wadau au wananchi wengi kutoa maoni inasaidia kuboresha sheria husika, ili inapoanza kutumika inakuwa haina makandokando mengi ambayo yataleta utata kwenye utekelezaji.

Ni muhimu sana wadau wanapoitwa kutoa maoni kuitikia wito, lakini muda wa kutoa maoni uwepo wa kutosha, ikiwamo njia mbalimbali zitakazohakikisha wananchi wengi wanasoma na kutoa maoni yao.

Wabunge ni wawakilishi wa wananchi, lakini muswada unapoletwa na serikali wanaujadili kwa kadri ya uelewa wao, ndiyo maana wananchi wanashirikishwa kupitia makundi yao kupeleka maoni ili sheria iwe shirikishi.

Mathalani, LHRC imebainisha kasoro nyingi kiasi cha kupendekeza kufutwa kwa kifungu kizima cha masuala ya ugaidi kwa kuwa itawapa shida sana Mahakama kutafsiri sheria huku ikitoa nafasi kwa watu kuonewa au kuumizwa baada ya kutangazwa kuwa ni magaidi na kuwekwa kwenye gazeti la serikali.

Pia walisema kuacha ilivyo kuitaipa Mahakama wakati mgumu kupima hofu au kutishika kwa umma, kwamba itatakiwa kuita mtu mmoja mmoja kumuhoji kama alitishika.

Walisema kama mtu akiwasha moto kwenye mtaa na kuzua taharuki kwa sheria hiyo atashtakiwa kama gaidi, na kwamba tatizo kubwa itakuwa kwenye utekelezaji.

Wadau hao wanasema sheria imeangalia maandamano ya kisiasa na kusahau kuwa kuna ya kidini na mengine ambayo ni ya taasisi husika, lakini sheria inakizana na katiba ambayo inaruhusu mikusanyiko.

Kama ambavyo wataalamu wa sheria wameona mambo mengi ikiwamo kuipa shida Mahakama na kuilazimu kwenda bungeni kupitia kumbukumbu za Bunge, ili kujua mbunge au wabunge walimaanisha nini kwenye jambo husika.


Ikiwa wananchi wengi watajitokeza kutoa maoni yao itasaidia kuwa na sheria shirikishi, lakini haitakuwa na malalamiko kwenye utekelezaji.

Kwa ujumla kuna mambo mengi ambayo yameibuliwa na LHRC yanaonyesha kuna tatizo kubwa kwenye namna ambavyo suala la ugaidi linatazamwa, sheria inayotungwa siyo kwa ajili ya wabunge bali kila Mtanzania hivyo ikiachwa na kupita ilivyo kutakuwa na shida kubwa.

Mathalani, madhara kwa nchi itakuwa ni pamoja na kutambulisha duniani kuwa ina magaidi wengi hivyo watalii, wawekezaji kuogopa kuja, huku taasisi za fedha kutoleta fedha kwa nchi ambayo imejitangazia kuwa na magaidi wa ndani.

Maofisa hao walisema ni muhimu sana sheria hiyo inapotungwa isiangalie matukio yaliyoko au yaliyowahi kutokea nchini, bali utekelezaji wa sheria husika, ili kuhakikisha hakuna madhara kwenye haki za binadamu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Janga la uhaba wa walimu linavyolazimisha 'twisheni'

**KARIBU** shule zote za umma za msingi na sekondari zinaelezwa kuwa zina uhaba wa walimu, hali hiyo inaathari, kwa sababu inasababisha wanafunzi kutofundishwa kikamilifu masomo kwa mujibu wa mtaala.

Kwa hiyo kuwaongozea gharama zaidi wazazi na walezi, kutafuta masomo ya ziada kwa watoto wao yakiwamo yale yasiyofundishwa.

Shule za sekondari ndizo zenye uhaba huo wa walimu wa kutisha, hali ambayo ni vyema ikatafutiwa ufumbuzi wa kudumu ili kuwapunguzia mzigo wazazi na walezi, lakini kupata wataalamu wa fani mbalimbali wa baadaye.

Uhaba huo wa walimu unazikumbuka shule nyingi, lakini Sekondari ya Kenswa iliyoko Halmashauri ya Nsimbo mkoani Katavi, ni miongoni mwa shule zenye tatizo hilo.

Taarifa zinasema walimu wanaohitajika ni 29, lakini walioko ni 10 pekee hali inayosababisha waelemewe na mzigo mkubwa wa kufundisha.

Shule nyingine yenye tatizo kama hilo, ni Magema Sekondari iliyoko Wilaya ya Geita mkoani Geita, ambayo imewahi kuripotiwa na ITV kuwa ina walimu wawili, katika taarifa ITV shule hiyo ilikuwa na walimu wawili, huku idadi kubwa ya wanafunzi wakikosa kufundishwa masomo mengine yakiwamo ya sayansi.

**Shule nyingine yenye tatizo kama hilo, ni Magema Sekondari iliyoko Wilaya ya Geita mkoani Geita, ambayo imewahi kuripotiwa na ITV kuwa ina walimu wawili, katika taarifa ITV shule hiyo ilikuwa na walimu wawili, huku idadi kubwa ya wanafunzi wakikosa kufundishwa masomo mengine yakiwamo ya sayansi.**

Hivyo baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo wanaiambia ITV na kuiomba serikali kuwaongezea walimu, kwa kuwa wawili waliokuwapo walikuwa hawatoshi kufundisha masomo yote, ni janga shule kuwa na walimu wa wawili, ukweli ni kwamba, si rahisi kufundisha wanafunzi masomo yote na badala yake wazazi na walezi itabidi wanalazimike kulipia watoto wao gharama za twisheni.

Uhaba huo unasababisha watafute walimu wa kuwafundisha watoto wao masomo wanayoyakosa shuleni, kwani mitihani ni wa masomo yote, bila kujali kwamba mengine hawajafundishwa.

Kwa hali kama hiyo ni wazi inabidi wazame zaidi mifukoni kutoa pesa ili kulipia masomo ambayo hayana walimu shuleni, hali ambayo ni wazi wanajikuta wakipata gharama ambazo wakati mwingine ziko nje ya bajeti.

Miongoni mwa masomo ambayo mara nyingi huwa hayana walimu ni ya sayansi kuanzia kemia, fizikia na baiolojia ambayo kwenye twishen' hutozwa kuanzia Shilingi 25,000 kwa somo moja.

Ninatambua kile ambacho serikali inakisema kuwa, inaendelea kupunguza uhaba wa walimu katika shule zake ili kukabiliana na upungufu wa watumishi nchini kadri ya mahitaji yatakavyojitokeza hasa walimu wa sayansi.

Inakiri kwamba, kwa nchi nzima uhaba wa walimu upo hasa kwa walimu wa sayansi, ambapo Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, anasema serikali itaendelea kutoa ajira hasa za walimu wa sayansi ili kupunguza upungufu huo wa walimu. Lakini swali linabaki tutangojea mpaka lini?

Ingekuwa ni vyema kama kasi ya kuajiri walimu wa masomo hayo, ikaongezeka ili kupunguzia wazazi gharama za twisheni, lakini kuandaa wataalamu wa kutosha wa fani mbalimbali hapo baadaye.

Ingependeza juhudi ambazo zimetumika kujenga madarasa na kuwafanya wanafunzi wote waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza mwaka huu kwa pamoja, zingetumika pia kuhakikisha shule zinakuwa na walimu wa kutosha ili kukabiliana na upungufu huo unaoathiri elimu.

# 22 mbaroni tuhuma za mauaji Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linawashikilia watu 22 wanaotuhumiwa kushiriki kwenye mauaji ya watu mbalimbali wakiwamo wanaotuhumiwa kumuua Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Mahabusu ya watoto kwa kumnyonga.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema watu hao walikamatwa kufuatia msako maalumu uliofanywa na makachero wa jeshi hilo.

Alisema jeshi hilo liliamua kufanya operesheni hiyo baada ya kuongezeka kwa wimbi la mauaji ya watu ndani ya mkoa huo yakiwamo yanayohusiana na visasi na wivu wa mapenzi.

Alisema katika tukio la mauaji ya Ofisa Maendeleo ya Jamii, Gloria Kibira (38) ambaye alikutwa amenyongwa ndani ya nyumba aliyokuwa anaishi ndani ya mahabusu ya watoto iliyoko Block T jijini Mbeya, watu wanne wanashikiliwa.

Aliwataja wahusika ni Catherine Chacha (26), Elia Mwakajinga (30) wote wakazi wa Majengo jijini Mbeya, Joseph Kiguha (39) mkazi wa Kilimanjaro na Banda Simkonde (45) mkazi wa Ilemi jijini Mbeya ambaye alikuwa Mlinzi katika eneo hilo.

"Marehemu aliuawa kwa kunyongwa shingo ndani ya nyumba yake Februari 3, mwaka huu saa 5:45 usiku, sasa hawa watu tunawashikilia kwa ajili ya upelelezi na mpaka sasa tunaendelea na mahojiano nao," alisema Kamanda Matei.

Watuhumiwa wengine wanane wanashikiliwa kwa tuhuma za kumuua aliyekuwa Mwenyekiti wa Mtaa wa Hasanga Kata ya Uyole jijini Mbeya kwa kumchoma na kisu kifuani.

Kamanda Matei aliwataja wanaoshikiliwa ni Seleman James (34), Shaban Mgani (19), Issa Kolelo (24), Abel Zuberi (19), Christopher Mwalingo (26), Yese Mwangosi (22), Ambakisye Victor (20) wote wakazi wa Uyole na Kenguard Ndele (24), mkazi wa Itezi.

Wengine wanaoshikiliwa ni wanaotuhumiwa kumuua Lwitiko Edson maarufu kwa jina la Imma mkazi wa Simambwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwa kumpiga sehemu mbalimbali za mwili.

Kamanda Matei aliwataja watuhumiwa hao ni Venance Melele (50), Rozen Ibrahim (27), na Amani Daniel (36) wote wakazi wa Simambwe, Shazian Philosy (30) na Kelvin Mazyo (45), wote wakazi wa Mji wa Mbalizi na Yotham Samwel (40) mkazi wa Utengule Usongwe.

Alimtaja mtuhumiwa wa mwisho ni Mussa Ndonde (31) ambaye anatuhumiwa kumuua baba yake mzazi Mzee Edward Ndonde (75) ambaye alikuwa ni mwalimu mstaafu kwa kumchoma na kisu.




Katapila likisawazisha udongo kwenye barabara ya Ukonga Mombasa kuelekea maeneo ya Kwa Diwani, jijini Dar es Salaam juzi. Kwa mujibu wa wakazi wa eneo hilo kifusi hicho kiliwekwa zaidi ya miezi miwili iliyopita bila kusawazishwa na kusababisha usumbufu kwao. **PICHA: SABATO KASIKA**

# W/biashara wafunguka kampeni ya TRA mlango kwa mlango

**Na Jenifer Gilla**

FEBRUARI mosi, 2022 serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilianzisha kampeni ya mlango kwa mlango kwa wafanyabiashara kwa ajili ya kutoa elimu ya kodi, kuwatambua walipakodi wapya na kuwasajili.

Lengo la shughuli hiyo ni kurahisisha usajili wa walipakodi wapya kwa kuwasogeza karibu huduma wafanyabiashara wote kwa kuwafuata katika maeneo yao ya biashara badala ya kuwasubiri waende kwenye ofisi za TRA.

Hatua hiyo imewaibua wafanyabiashara pamoja na wadau wa masuala ya kodi na kutoa maoni yao kuhusu mchakato huo. Mfanyabiashara wa nguo za jumla katika Soko la Kariakoo, Bertha Mmari, alisema elimu ya kulipa kodi itawasaidia wafanyabiashara kuwa na mwako wa kutoa kodi kwa sababu watajua matumizi ya pesa ile na faida yake kwa jamii.

"Unajua wafanyabiashara wengi wanaua kuwa ile pesa wanayotoa labda inatumika kwa mambo yasiyo ya lazima, mfano kulipa mishahara ya wafanyakazi wa TRA tu, kumbe peaa nyingine zinapelekwa kwenye miradi ya maendeleo kama kujenga shule, kwa hiyo elimu kama hii tunaihitaji ili itupe msukumo wa kulipa kodi kwa hiyari," alisema Bertha.

Naye mfanyabiashara wa jumla wa pochi katika soko hilo, Irena Thomas, aliusifia uamuzi wa TRA kutembelea wafanyabishara na kuwasajili kwa kuwa wengi wanashindwa kwenda kujisajili ofisini kwao kutokana kwa kutojua waanzie wapi.

"Sio kwamba wafanyabiashara hawataki kulipa kodi, ila wengi hawana elimu ya mchakato mzima wa kulipa kodi, kwamba aanzie wapi na amalizie wapi, na pia kwenye ofisi zao usumvufu ni mwingi.

"Unaweza kutumia wiki nzima unafuatailia cheti tu TIN namba, wakitufuata kwenye biashara zetu kutupa elimu na kutusaidia kujisajili watakuwa wametusaidia sana."

Antony Mmasi, muuza duka la jumla Mwenge Sokoni, alisema wakati mwingine wanabanwa na majukumu ya biashara zao na h kujisahau kulipa kodi, hivyo uamuzi wa TRA utasaidia wafanyabiashara wengi kulipa kodi kwa wakati.

"Lakini pia baada ya kutembelea na kutusajili wawe wanatutumia na meseji kwenye simu za kutukumbusha kulipa kodi hii itatusaidia kulipa kwa wakati kwa kuwa saa nyingine tunasahau kwa kutingwa na majukumu," alisema.

Aloyce Julius, mfanyabiashara wa vifaa vya umeme eneo la Posta, anashauri kuwa mchakato huo uwe endelevu ili uwe na tija ya muda mrefu.

"Ili mchakato huu uwe endelevu serikali iufanye uwe endelevu mpaka pale itakapijiridhisha kuwa suala la ulipaji kodi limekaa kwenye mstari, kwa sababu serikali ina abia ya kuanzisha jambo na kuliacha katikati,,"alishauri Aloyce.

Naye mchumi Dk. Abel Kinyondo, Mhadhiri Mwandamizi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alisema ulipaji kodi ni kitu muhimu kuwa hunufaisha pande mbili, serikali na mlipakodi mwenyewe kwa kuwa matumika katika shughuli za maendeleo ya nchi .

"Fedha zinazokusanywa ndio hulipa mishahara ya polisi ambao wana jukumu la kusimamia usalama wa nchi ikiwamo wafanyabiashara na bidhaa zao, kuboresha huduma za kijamii kama shule na hospitali, njia wanazotumia kusafirisha bidhaa zao ikiwamo barabara na reli zimetengenezwa kwa kutumia pesa za kodi." alisema.

Aliongeza kuwa kutolewa kwa elimu humfanya mfanyabiashara kuelewa vizuri, kama alikuwa anadanganywa kuwa tayari kulipa tozo sitahiki.

# NMB sasa yawapa ahueni wanawake wenye biashara

**Na Christina Mwakangale**

BENKI ya NMB imezindua mpango maalumu wenye ahueni kwa wanufaika wa mikopo kibiashara na kampuni zinazomilikiwa na kusimamiwa na wanawake na biashara ambazo bidhaa zake ni huduma zinazomnufaisha mwanamke.

Ofisa Mtendaji Mkuu NMB, Ruth Zaipuna, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akitangaza kuanza kuuzwa rasmi kwa hati fungani, iitwayo NMB Jasiri.

Zaipuna alisema hati hiyo ya miaka mitatu, ni kwa ajili ya wawekezaji wote, wakubwa na wadogo na kwa mtu yeyote aliye tayari kuwekeza kwenye benki hiyo, akisema lengo ni kusaidia biashara za wanawake.

"Hati fungani hii, itawapatia riba nzuri ya asilimia 8.5 kwa mwaka. Kiwango cha chini cha ununuaji wa hati fungani ni Sh. 500,000 na unaweza kununua kupitia tawi lolote la NMB au kupitia kwa madalali waliosajiliwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA).

"Tunategamea kupata jumla ya Sh. bilioni 25 kupitia mauzo ya hati hii, ambayo pia ina kipengele cha kuongeza Sh. bilioni 15 zaidi," alisema Zaipuna.

Kuhusu mapato ya hati hiyo, Zaipuna alibainisha, mpango huo utatumika kusaidia utoaji wa mikopo nafuu kwa biashara, kampuni zinazosimamiwa na wanawake huduma ambayo ni ya kwanza kutolewa kibenki kwa ukanda wa Afrika Mashariki, mahsusi kwa ajili ya wanawake, kijamii na kiuchumi.

"Benki ya NMB inaendelea kuunga mkono juhudi za kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), hasa lengo namba tano, linalohusu usawa wa kijinsia na lengo namba 10 kuhusu kupunguza tofauti za kijinsia.

"Wawekezaji kwenye hati fungani hii, watapata riba ya asilimia 8.5 kwa mwaka, itakayolipwa kila robo mwaka, wakati wa kipindi chote cha miaka mitatu, hadi Machi mwaka 2025. Riba itakayolipwa itakatwa kodi ya zuio," alieleza Zaipuna.

Alielezea kwamba NMB Jasiri, ni matokeo ya kibali kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kuruhusu awamu ya nne ya Programu ya NMB ya utoaji wa hati fungani ya muda wa kati, yenye thamani ya Sh. bilioni 200 na kwamba awamu ya tatu iliwezesha kupatikana kwa Sh. bilioni 148.2. "Kupitia hati fungani, tunaonyesha kwa vitendo jinsi ya kuzitatua changamoto ambazo wajasiriamali wanawake wa Tanzania wanakabiliana nazo, kwetu sisi hii ni fursa ya kukabiliana na changamoto hii.

IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL
FOR MARA
AT MUSOMA

MISC. APPLICATION NO. 1136 OF 2021
(Arising from the judgment of case no. 4/2018 at DLHT- Musoma )

TUJIJENGE TANZANIA .......................................... APPLICANT
VERSUS
1. KICHERE NGOCHOGE
2. TWALIB ALLY .............. RESPONDENTS

**SUMMONS/NOTICE**

**TO,**
**KICHERE NGOCHOGE**
**TWALIB ALLY**
The above mentioned applicant has instituted a suit in this Tribunal, against you, particulars of which are mentioned in a copy of the Application which is obtainable from the registry of this Tribunal. **YOU ARE HEREBY SUMMONED TO APPEAR IN THIS TRIBUNAL** in person (s) or by recognized agent(s) for mention on 14TH February, 2022 at 08:00am in the fore noon.

**TAKE NOTICE THAT;**
In default of your appearance on the said day, the above mentioned suit shall be mentioned and determined in your absence.

Given under my hand and seal of this Tribunal this ....31.......... day of January.........., 2022.

Kitungulu Elias
Chairman
The District Land and Housing Tribunal – Mara

THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL MUSOMA

166932

# Sheria mpya utakatishaji wa fedha yapendekezwa

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimependekeza kutungwa upya kwa Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu, kwa kuwa mabadiliko yanayopendekezwa ni mengi.

Akiwasilisha maoni hayo mwishoni mwa wiki katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Ofisa Uchechemizi wa LHRC, Raymond Kanegele, alisema mwishoni mwa wiki kuwa sheria hiyo ina marekebisho makubwa yanayopaswa kufumuliwa na kutungwa upya. Muswada huo utakaojadiliwa leo bungeni, unapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu, Sura ya 423, na kufanya marekebisho sheria nyingine tano ikiwamo ya kuzuia ugaidi.

"Ni muhimu tuwe na sheria mpya. Sheria ina mchanganyiko," alisema na kusisitiza kuwa sheria itarahisisha mahakama katika kuitafsiri.

Akijibu swali la mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria, Halima Mdee kuhusu mtazamo juu ya adhabu zilizopendekezwa na marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Ugaidi (Sura ya 19) , Ofisa Programu wa LHRC, Maduhu William alisema ziko vizuri.

Alisema makosa yaliyopendekezwa mengi ni mapya na wameridhishwa na hatua ya mapendekezo kuweka adhabu ya kifungo pamoja na faini tofauti na sheria mama ambayo ina kifungo pekee.

Mjumbe wa kamati hiyo ambaye ni Mbunge wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina aliwashukuru LHRC kwa ufafanuzi huo.

Naye Mjumbe wa Kamati hiyo ambaye Mbunge wa Sikonge (CCM), Joseph Kakunda, alisema: "Sasa hii si kazi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), wanatakiwa wafanye upelelezi wa kutosha wakathibitishe kosa mahakamani, kwanini tuweke mpaka kwenye sheria?"

Kuhusu kumtangaza mtu kuwa gaidi wa ndani, alisema anapendekeza kifungu hicho kisifutwe bali waziri awekewe mwongozo wa kutunga kanuni ili watu wasionewe kwa kutangazwa magaidi.

Akijibu hoja hiyo, Kenegela alisema: "Mara kadhaa mahakama inaingia kwenye mkwamo, inatakiwa iongozwe kufikia kutenda haki ina DPP na upande wa utetezi ambao wanatumia sheria, lazima uthibitisho uongozwe na sheria kuwawezesha, lazima kuwe na sheria ya kuiongoza mahakama ili ifikie sehemu nzuri ya kutoa haki.

Naye Maduhu alisema sheria nyingi ziko kimya kiasi kwamba inailazimu mahakama kwenda bungeni kusikiliza kumbukumbu za Bunge ili kujua ilidhamiria nini kabla ya kufikia maamuzi kwa mujibu wa sheria.

Alisema kwa jinsi sheria ilivyo kwenye masuala ya ugaidi, kufadhili na kusafirisha binadamu mahakama itashindwa kufikia maamuzi na itawalazimu kuja kusikiliza kumbukumbu za Bunge kujua mbunge mmoja mmoja alimaanisha nini kwenye jambo hilo.



Wananchi wakiwa kwenye foleni ili kupata huduma ya uchunguzi wa afya bure iliyotolewa na kituo cha Kairuki Polyclinic katika kituo cha mabasi cha Magufuli Mbezi Luis jijini Dar es Salaam, ikiwa ni kumbukumbu ya miaka 23 ya kifo cha Prof. Hubert Kairuki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Walia kukosa matibabu zahanati mwisho wa wiki

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI wa Kijiji cha Shilabela wilayani Shinyanga, wamelalamikia zahanati ya kijiji hicho kusitisha huduma ya matibabu siku za Jumamosi na Jumapili.

Wamesema wamekuwa wakipata shida ya huduma za matibabu, na kuamua kwenda kutibiwa kwenye maduka ya dawa ya watu binafsi na kupewa dawa bila ya kupimwa ili kujua magonjwa yanayowasumbua.

Walibainisha hayo kwa nyakati tofauti wakati wakizungumza na Nipashe, katika kutekeleza mradi wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, ambao unaendeshwa na klabu ya waandishi wa habari mkoani Shinyanga, kwa ufadhili wa Mfuko wa Ruzuku wa Wanawake Tanzania (WFT).

Matha Tungu, alisema siku hizo wamekuwa wakipata shida ya matibabu, ambapo zahanati yao huwa haitoi huduma za matibabu, na kuiomba serikali iwasaidie isiwe inafungwa kwa ajili ya kuokoa afya zao.

"Wananchi wa Shilabela tunapata shida sana ya matibau Jumamosi na Jumapili, ambapo zahanati ya kijijini hapa haitoe huduma za matibabu," alisema Tungu.

Naye Diwani wa Pandagichiza, Charles Kabogo, alithibitisha kupokea malalamiko ya zahanati hiyo kufungwa siku za wikiendi, na kubainisha kuwa siku moja alifuatwa na mwananchi akimwomba msaada wa pikipiki ili ampeleke mtoto wake kwenda kutibiwa Shinyanga Mjini na alimpatia.

"Lengo la serikali kujenga zahanati karibu na wananchi ni kuwasaidia wapate huduma za matibabu na kuokoa afya zao... sasa inapofungwa siku za wikiendi sijui ndiyo wananchi hawaugui, ninacho kiomba zahanati hiyo isifungwe tena," alisema Kabogo.

"Zahanati ya kijiji hiki ina hudumia wananchi wote wa Kata ya Pandagichiza katika vijiji vinne, sababu vijiji vingine havina zahanati ndiyo zipo kwenye hatua za ujenzi, hivyo ikifungwa ni kuumiza wananchi," aliongeza.

Mganga Mkuu wa Zahanati hiyo, Nassoro Ahmed, alisema Jumamosi na Jumapili kuwa wanatoa huduma hadi saa sita mchana.

Aidha, alisema kwa wagonjwa wa dharura wakiwamo wajawazito hufuatwa majumbani mwao ambapo ni karibu na zahanati na kisha kuwapatia huduma, na kubainisha kuwa huwa wanafunga zahanati siku hizo kutokana na kuchoka kwa kuwa wapo wauguzi watatu na kwa siku moja wanahudumia watu 30 hadi 40.

# Shirika lajitosa kuhimiza chanjo ya UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Himiza Development Organization, linalohudumia watoto na wanawake, limetenga siku ya Alhamisi kwa ajili ya kutoa elimu mbalimbali kwa jamii, lakini kuhimiza chanjo ya UVIKO-19.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Prisca Ng'weshemi, aliliambia gazeti hili jana kuwa limechukua hatua hiyo kwa kuwa yeye na viongozi wenzake ni sehemu ya jamii, na kwamba hawana budi kuunga mkono maelekezo ya serikali.

"Kila Alhamisi huwa ni ya mdahalo, tunakwenda katika jamii, kujadili mada mbalimbali zikiwamo za ukatili wa kijinsia na haki za watoto na wanawake, lakini tunatumia nafasi hiyo kuhimiza chanjo ya corona," alisema Prisca.

Alisema, makao makuu ya shirika hilo yapo Kata ya Kitunda Dar es Salaam, na kwamba mbali na hayo, jamii katika eneo hilo imekuwa ikipata pia msaada wa kisheria inapokumbana na vitendo vya ukatili.

"Katika midahalo yetu, huwa pia tunaikumbusha jamii kuwa ukatili ni mpana, kwani hata kutompa mtoto au mwanamke mahitaji yake ya msingi ni ukatili wa kijinsia, katika utoaji wa elimu hiyo, tunachombeza suala la chanjo," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema, shirika lake linaamini kuwa chanjo ni salama, na kwamba, ndiyo maana likaamua kuingiza suala la kuhimiza chanjo ya UVIKO-19 kwenye mdahalo wa kila Alhamisi.

Alifafanua kuwa wamekuwa wakizunguka kila kitongoji katika Kata ya Kitunda na kukusanya wananchi na kuweka mdahalo na kwamba, kabla ya kufunga huwa wanawaeleza kwenda kuchanjwa.

"Jambo la msingi ni kwamba kila Mtanzania anatakiwa kutambua kuwa suala la chanjo ya corona halikwepeki na pia kuna haja kuachana na elimu ya mitaani inayopingana na chanjo," alisema.

Alisema, suala la kuhimiza chanjo ya ugonjwa huo si la serikali tu bali kila Mtanzania kwa nafasi yake anatakiwa kumwambia mwenzake aende kuchanjwa ili kuwa salama zaidi.

Prisca alisema, serikali imeshatoa maelekezo ukiwamo mwongozo wa kujikinga na ugonjwa huo, na kwamba shirika lake linaunga mkono juhudi zote zinazolenga kuhakikisha Watanzania wanakuwa salama.

# Mradi unavyowanufaisha wakulima Nyanda za Juu

**Na Friday Simbaya,** KILOLO

MIKOA minne ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini imefaidika na mradi wa kampuni ya One Acre Fund ambayo imekuwa ikitoa mikopo ya pembejeo na kuunga mkono serikali kupitia kampeni ya upandaji wa miti.

Ofisa Mawasiliano wa One Acre Tanzania Ltd, Dorcas Tinga, alisema wakati wa ugawaji wa miti kwa wakulima wa Wilaya ya Kilolo katika kijiji cha Luganga mkoani Iringa kuwa wanajihusisha na ukopeshaji wa pembejeo huku akibainisha kuwa msimu huu wameweza kuwafikia wakulima zaidi ya 100,000.

Alisema wamesambaza miche zaidi ya milioni moja kwa wakulima wanaoishi mikoa mitatu ya Iringa, Mbeya, Njombe na Songwe katika kuunga juhudi zinazofanywa na serikali ili kuwahamasisha wakulima kupanda miti zaidi kuliko kutegemea zaidi kilimo cha mahindi.

"Msimu huu tunatoa huduma ya miche ya miti inayotumika kuboresha ardhi ili kupunguza changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa, matunda ambayo yamekuwa msaada mkubwa kwa baadhi ya wakulima na mbao ambazo zitamsaidia kuondokana na changamoto za kipato mkulima asitegemee tu mahindi ... tunaamini zitakuwa na msaada kwa wakulima," alisema.

Alisema kuwa kutokana na serikali kutangaza soko la parachichi India, wameitumia fursa hiyo kwa kutambua umuhimu wa kumwezesha mkulima kwa kumkopesha miche ya matunda mbalimbali.

"Parachichi kwanza sasa hivi ni zao la kimkakati kwa hiyo tunaamini sana sisi kwa wakulima kupanda parachichi zaidi itawasaidia wao pia kupata masoko... mwaka jana serikali ilitangaza limepatikana soko la parachichi India, tunaamini hizo ni fursa," alisema.

Dorcas alisema kuwa walikuwa wakiwakopesha wakulima pembejeo ambazo wamekuwa wakirejesha ndani ya mwaka kutegemeana na muda waliokopeshwa ili kumwekea mkulima utaratibu mzuri utakaomwezesha kulipa kidogo kidogo hadi atakapomaliza.

Kauzeni Kikot, Mkurugenzi Idara ya Mashamba Mkoa wa Iringa, aliwataka wakulima kupanda na kuisimamia miche ya matunda ili kuwapatia faida kwani ndani ya miaka mitatu kuna uwezekano mkubwa wa matunda kuanza kuzaliana kutokana na miche hiyo kukua chini ya usimamizi wa ofisa kilimo kutoka katika kampuni hiyo.

Alisema matunda hayo yatawasaidia wakulima kupata kipato endapo itatunzwa vizuri, itasaidia pia kuongeza lishe katika familia, huku akibainisha kutoa miche ambayo itasaidia katika urutubishaji wa ardhi miche ya mbao kutokana na hitaji la mkulima.

"Tutunze kwa ajili ya afya zetu, tunaweza tukauza tukapata matunda, lakini hata kwa ajili ya lishe kwenye familia zetu tutapata," alisema.

Rebecca Makukuru, mnufaika anayewezeshwa na One Acre Tanzania, alisema kampuni hiyo imekuwa ikiwasaidia kutokana na kutoa mbolea nzuri na kuweka masharti nafuu ambayo yanampa mkulima nafasi ya kujikimu kidogo kidogo na kwamba ni mmoja wa wanufaika wa mradi wa miti ya mbao iliyotolewa na kampuni hiyo. "Toka mradi huu umeanza umetusaidia sana sisi wananchi wa Luganga, kwanza mbolea yake ni nzuri pili tunapata mbolea ile kwa kulipa kidogo kidogo. Pia inamsaidia mkulima mkopo, nimeona nichukue kwa sababu hii miti ina faida mbeleni hata isiponinufaisha mimi watanufaika kizazi kijacho," alisema.

Mnufaika mwingine, Agustino Mwanza, alisema lengo la kuchukua miche ya parachichi aliona umuhimu wake kutokana na kuwa ni miche endelevu ambayo hudumu kwa kizazi hata kizazi tofauti na miti ya mbao ambayo mkulima anavuna baada ya miaka kumi na kupanda kwa wakati mwingine atakapokuwa amevuna.

## M/kiti afichua wazazi, walezi kuwatumikisha watoto wao

**Na Yasmine Protace**

MWENYEKITI wa Serikali ya Mtaa Amani Kata ya Kipunguni mkoani Dar es Salaam, Donald Malaghashimba, amewaonya wazazi na walezi ambao uwatumikisha watoto wadogo wa shule kazi za kuuza mboga ambazo huzibeba kichwani zikiwa katika mabeseni.

Malaghashimba aliyasema hayo, katika Club ya Kipunguni ambayo iliandaa mafunzo ya kupiga vita ukatili ndani ya jamii.

Malaghashimba ambaye alikuwa ni mgeni rasmi katika mafunzo hayo, alisema kuwa ukatili unaanzia nyumbani kwa wazazi na walezi.

"Kuna wazazi na walezi ambao huwafanyia ukatili watoto kwa kuwabebesha mabeseni ya mboga vichwani na kuzunguka nayo kwa kuuza mboga hizo," alisema.

Aliongeza kuwa anakerwa na tabia hizo, badala mtoto asome yeye anatembeza mboga.

Aliongeza kuwa watoto ambao wanafanyiwa ukatili wafike kwake watoe taarifa ili mhusika achukuliwe hatua.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Taarifa na Maarifa cha Kipunguni, Selemani Bishagazi, alisema kuwa wamekuwa wakitoa elimu ya masuala ya ukatili lengo kuwawezesha jamii kupata elimu hiyo ambayo itakuwa mkombozi kwao.

Prisca Ngomelo, kutoka taasisi inayoshughulika na masuala ya ukatili wa kijinsia (IMIZA), alisema ukatili upo mwingi ila wanaofanyiwa matendo hawatoi taarifa.

Jackison Malangaiila kutoka TGNP Mtandao, alisema kuwa wamekutana na wanajamii ili kuzungumzia masuala ya ukatili.

Alisema kuwa Kipunguni ni kata ambayo ina matukio mengi ya ukatili.

Alisema wanahabari, wanaharakati na jamii kwa umoja wao wanatakiwa kupiga vita masuala ya ukatili ukiwamo ukeketaji.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zinapambana na masuala ya ukatili na ukeketaji.



Baadhi ya wanajamii wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE) wakifuatilia hotuba ya Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Makundi Maalum, Mwajuma Magwiza (hayupo pichani), wakati wa uzinduzi wa Dawati la Jinsia chuoni hapo jana. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Wanaume waitwa kupima tezi dume bure

**Na Joseph Mwendapole**

WANAUME wenye umri wa miaka 40 na kuendelea wameshauriwa kujitokeza kwa wingi kupima saratani ya tezi dume bila malipo ambayo yanatolewa mwezi mzima ili watakaokutwa na matatizo waweze kupatiwa tiba mapema.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mganga Mkuu wa Manispaa ya Ubungo, Dk. Peter Msanya, wakati wa ufunguzi rasmi wa Kituo cha Kairuki Polyclinick kilichoko Kituo cha Mabasi cha Magufuli Mbezi Luis.

Kituo hicho kiliendesha kambi ya uchunguzi wa afya na matibabu bure kwa siku mbili kama sehemu ya kumuenzi mwanzilishi wa mtandao wa KHEN, Prof. Hubert Kairuki aliyefariki miaka 23 iliyopita na sasa kimeongeza muda wa kupima saratani ya matiti na tezi dume hadi tarehe 28.

Alisema uchunguzi wa saratani ya tezi dume unafanywa kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya mashine ya ultrasound tofauti na njia ya awali ya kutumia kidole iliyokuwa ikiwaogopesha wanaume wengi kujitokeza.

Badala ya kukaa bila kujua hali yako nawasihi sana wanaume wenye umri wa miaka 40 na zaidi kutumia fursa hii ili kutambua afya zenu mapema tena ni bure na nimeambiwa huduma hii ya bure itaendelea kutolewa bila malipo hapa Kairuki Polyclinic hadi tarehe 28 mwezi huu, tafadhali sana wananchi tutumie fursa hii, alisema.

Alisema kupima afya mara kwa mara ni utamaduni mzuri ambao kwa bahati mbaya umeenea sana nchi za magharibi kuliko hapa nyumbani Tanzania.

Alisema hali hiyo imechangiwa kwa kiasi kikubwa na changamoto za upatikanaji wa huduma za afya na pia utamaduni wa Watanzania wengi ambapo mtu hupima afya pale anapougua.

Pamoja na hayo nakipongeza sana kituo chenu cha Kairuki Polyclinic kwa kutoa huduma hizi za kupima afya bila malipo na kuwapa wananchi elimu pamoja na ushauri wa kitabibu unaosaidia kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kupima afya zao ili kufahamu magonjwa mbalimbali na namna ya kujikinga, alisema.

„Nimesikia ushauri wa kitabibu kuwa uwiano kati ya uzito na urefu yaani "Body mass index" na Shinikizo la damu ni hali inayotokana na mfumo wetu wa maisha tunayoishi na aina za vyakula tunavyokula hivyo tunaweza kabisa kupunguza idadi ya wagonjwa wa magonjwa ya moyo kama tukizingatia ushauri wa wataalamu wa afya," alisema.

Aliuomba uongozi wa taasisi za Kairuki uendelee kusaidia jamii ya Tanzania kwa kuhakikisha kuwa inaendelea kuwa na afya njema na taarifa sahihi juu ya magonjwa na namna ya kujikinga na magonjwa mbali mbali.

Mwenyekiti wa Mtandao wa Afya na Elimu wa Kairuki, (KHEN), Kokushubila Kairuki, alisema Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU), kimefanikiwa kutoa madaktari 1,512 tangu kuanzishwa kwake.

Alisema HKMU imeendelea na Chuo cha Uuguzi cha Kairuki, wameendelea kufundisha madaktari na wauguzi mahiri ambapo kufikia mwisho wa mwaka jana walishafikia idadi ya wahitimu zaidi ya Madaktari wa Shahada ya kwanza 1,512 na Madaktari Bingwa 63, wauguzi 1,205 Washauri Nasaha 205, ambao wanatoa huduma katika hospitali mbalimbali za umma na za binafsi.

# Serikali: Kiwira inaendelea kuchimba makaa ya mawe

BUNGE limeelezwa kuwa kwa sasa mgodi wa makaa ya mawe Kiwira unaendelea na uchimbaji kwa matumizi ya viwanda katika eneo la Kabulo na kuyauza kwenye viwanda mbalimbali vya saruji nchini.

Wizara ya Madini ilitoa majibu hayo jana bungeni katika swali la Mbunge wa Viti maalum, Sophia Mwakagenda.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini mgodi huo utapata mwekezaji mpya na lini waliokuwa wafanyakazi wa mgodi huo watalipwa mafao yao.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema serikali iliamua kuchukua hatua za ndani za kuendesha mgodi wa Kiwira kwa ajili ya uwekezaji mkubwa wa uzalishaji umeme wa Megawati 200 badala ya kutafuta mwekezaji mpya.

Ilisema hatua hizo ni pamoja na kufanya ukarabati wa miundombinu ya mgodi kwa kuboresha barabara, kurejesha njia za reli katika mgodi wa chini, mifumo ya hewa, maji na matengenezo ya mikanda ya kusafirishia makaa kuja nje ya mgodi.

Ilibainisha kuwa hatua hiyo ni kuwezesha kuchimba makaa ya mawe kwa wingi kwa ajili ya kuzalisha umeme na matumizi mengine na ukarabati wa miundombinu ya mgodi umefikia asilimia 98.

Aidha, ilisema hatua nyingine iliyochukuliwa na Serikali ni kuanzisha ushirikiano wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Shirika la Umeme nchini (TANESCO).

Katika ushirikiano huo, wizara hiyo ilisema STAMICO itahusika na uzalishaji wa makaa ya mawe kwa ajili ya matumizi kwenye kinu cha umeme na TANESCO itahusika na ujenzi wa kinu cha kuzalisha umeme pamoja na miundombinu yake.

Kadhalika, ilisema TANESCO watahusika na uzalishaji na usambazaji wa umeme kwa wananchi kwa kujenga njia ya umeme yenye urefu wa kilometa 100 kutoka kwenye mgodi huo.

Kuhusu malipo ya mafao ya waliokuwa wafanyakazi wa mgodi huo, wizara hiyo ilisema Wizara ya Fedha na Mipango inayafanyia kazi kufuatia kukamilika kwa uhakiki.

Ilifafanua kuwa madai hayo yanahusisha stahiki na mapunjo ya watumishi waliokuwa wafanyakazi wa mgodi huo uliokuwa umesimamisha uzalishaji wake mwaka 2007.

Hata hivyo, ilisema katika kipindi hicho mgodi ulikuwa unaendeshwa na kampuni binafsi ya TANPOWER na mwaka 2013 mgodi huo ulikabidhiwa na serikalini kupitia STAMICO



Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge Wanawake, Sally Raymond (kulia), akimkabidhi zawadi Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ikiwa ni ishara ya kumpongeza kwa kuchaguliwa kuwa spika, hafla hiyo iliyofanyika ukumbi wa Msekwa bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Taarifa ya tathmini mifuko uwezeshaji wananchi mbioni

SERIKALI imesema ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha taarifa ya tathmini ya mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na itawasilisha bungeni baada ya kukamilika.

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, ilibainisha hayo bungeni jana ilipokuwa ikitoa majibu kwenye swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Ng'wasi Kamani.

Katika swali lake, Kamani alihoji serikali imefikia hatua gani katika kufanikisha agizo lililotolewa na Rais wa Awamu ya Tano ya kuunganisha mifuko hiyo na kuwa na eneo moja la wazi la utoaji huduma ili kuwafungulia fursa wananchi kunufaika na mifuko hiyo bila vikwazo tena.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema inasimamia Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya Mwaka 2004 na Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya Mwaka 2004.

Aidha, ilisema serikali inaratibu utekelezaji wa mifuko na programu za uwezeshaji 62 ambapo mifuko na proramu 52 zinazomilikiwa na serikali na mifuko na programu 10 zinamilikiwa na taasisi za sekta binafsi.

Ilisema kati ya mifuko na proramu 52 zinazomilikiwa na serikali, mifuko 21 inatoa mikopo moja kwa moja kwa walengwa, mifuko tisa inatoa dhamana ya mikopo, mifuko 17 inatoa ruzuku na programu tano ni za uwezeshaji ambazo zinatoa huduma mbalimbali ikiwamo ujuzi, urasimishaji ardhi na uwekezaji.




## Uhakiki wa madai mawakala mbolea hatua za mwisho

WIZARA ya Kilimo imesema uhakiki wa madai ya mawakala wa mbolea za ruzuku upo katika hatua za mwisho.

Wizara hiyo iliyasema hayo bungeni jana ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Kalenga (CCM), Jackson Kiswaga.

Katika swali lake, Mbunge Kiswaga alihoji kwanini serikali isiwalipe angalau robo ya madai ya mawakala wa mbolea za ruzuku katika Jimbo la Kalenga kwa kuwa suala la uhakiki wa madai yao limechukua muda mrefu na hivyo kuathiri maisha na uchumi wao.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema mara uhakiki ukikamilika malipo hayo yatafanyika.

Ilisema serikali inatambua uwepo wa madai ya mawakala walioshiriki katika utoaji wa rukuzu ya pembejeo za kilimo kwa msimu wa 2014/15 na 2015/16 katika maeneo mbalimbali nchini ikiwamo Kalenga.

Ilibainisha kuwa wakati wa utekelezaji wa mpango wa ruzuku, uhakiki wa awali uliofanyika ulibaini kuwapo kwa udanganyifu.

Ilisema serikali iliamua kuchukua hatua za kufanya uchunguzi na uhakiki wa kina ili kubaini kiasi halisi cha fedha kinachopaswa kulipwa.

## Ahoji umeme REA kusuasua Makete

MBUNGE wa Makete (CCM), Festo Sanga, amesema Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini (REA) wilayani Makete umekuwa ukisuasua ambapo utekelezaji wake upo chini ya asilimia 50.

Akiuliza swali bungeni jana, Sanga alihoji Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha umeme huo unafika kila kijiji.

Katika majibu ya Wizara ya Nishati, ilisema Wilaya ya Makete ina jumla ya vijiji 93 na vijiji 56 vimekwisha fikishiwa umeme.

Hata hivyo, ilisema vijiji 37 ambavyo havikuwa na umeme vinapatiwa umeme kupitia mradi wa REA awamu ya tatu mzunguko wa pili unaoendelea kutekelezwa na Mkandarasi M/S JV Silo Power Limited & Guangzhou Yidian Equipment Installation Co. Ltd.

Ilifafanua kuwa mkandarasi anaendelea na kazi ya usanifu wa kina, upimaji, uandaaji wa michoro na manunuzi ya vifaa.

Ilisema mradi huo katika Wilaya ya Makete unahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo kilovoti 33 zenye urefu wa kilomita 222.5, kilomita 37 ya njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4, ufungwaji transfoma 37 za KVA 50 na kuunganisha wateja wa awali 814.

Ilieleza kuwa gharama ya mradi ni Sh. bilioni 9.95 na utekelezaji unatarajiwa kukamilika Desemba, 2022.

Nipashe
# TESA
Jumanne Februari 8, 2022
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Ukurasa 14



**Nape anapotangaza mazingira mapya sekta ya mawasiliano**



Ukurasa 13

Dar inapotakata mtihani la saba 2021

ELIMU

**NA MARCO MADUHU, SHINYANGA**

# Ukosefu taulo za kike bado kitendawili kinachotesa wasichana shule za vijijini

KUWAPO na taulo za kike kunaweza kupunguza utoro kwa wanafunzi kwa vile mabinti hushindwa kujisitiri wakati wa hedhi kumekuwa sababu mojawapo ya wasichana kutohudhuria masomo kikamilifu.

Changamoto hiyo ya ukosefu wa pedi inatatuliwa kwa juhudi kubwa mijini, lakini kwa wanafunzi wa vijijini linabakia kuwa tatizo kubwa ambalo pengine serikali ya awamu ya sita inapaswa kulitazama kwa jicho la kipekee na kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kuzalisha taulo hizo kwa wingi.

Ukosefu huo, umeendelea kuwakwamisha wanafunzi wa vijijini, maeneo ambayo upatikanaji wa huduma hiyo ni mgumu, lakini ugumu wa maisha unaowakwamisha wazazi na walezi kushindwa kuzinunua.



Mahitaji ya pedi na kuwapo hedhi salama lisipate kigugumizi bali liwe huduma muhimu inayopatikana kwa kila mwanamke. **PICHA: MTANDAO.**

Baadhi ya wasichana wa shule za msingi na sekondari kutoka vijiji vya Sayu, Ng'wamadelanha, Shilabela, pamoja na Pandagichiza wilayani Shinyanga, ambao wanawakilisha wanafunzi wa maeneo mengi ya vijijini wanasema wanaendelea kukwamishwa na ukosefu wa taulo za kike na vyoo kwa ajili ya kujistiri wakati wa hedhi.

Wanapozungumza na Nipashe wanasema kwa maeneo mengi Tanzania suala la hedhi linachukuliwa kama mwiko au bado ni jambo la siri si wazazi, walezi na jamii inalolizungumzia. Wanalifanya kuwa siri nalisilostahili kutoka nje ya jamii ya kinamama licha ya kuathiri maendeleo na afya ya taifa.

Wanasema bila hedhi salama, afya ya uzazi iko hatarini lakini hata watoto wanaozaliwa hawawezi kuwa na afya timamu pia.

Mwanafunzi Scholastika Madatula anayesoma darasa la saba katika Shule ya Msingi Pandagichiza wilayani Shinyanga, anasema kutokana na maeneo hayo ya vijijini upatikanaji wa taulo za kike kuwa mgumu, pamoja na wazazi na walezi kushindwa kuzimudu, wanalazimika kutumia njia za asili kujistiri ambazo si salama.

Anasema baadhi ya mbinu hizo ni kutumia vitambaa ili wasikose vipindi darasani na kuendelea kufanya vizuri kitaaluma licha ya kukabiliwa na changamoto hiyo.

Anaungwa mkono na Felister Jilala ambaye anayesoma darasa la saba katika shule hiyo, anayaeleza kuwa wanakutana na changamoto nyingi kutokana na ukosefu wa pedi na wakati mwingine wanalazimika kutumia hata karatasi za vyooni (toileti papers) na leso.

"Hapa shuleni kwetu hatuna vyoo kwa ajili ya kujistiri, lakini familia zetu hazina uwezo wa kuzinunua kutoka mjini, hivyo ni changamoto kiafya, kielimu na hata kimazingira kwani kama hakuna sehemu ya kutupa taka za hedhi mwanafunzi anakuwa na wakati mgumu zaidi," anasema Felister.

Mariamu Kashinje mwanafunzi mwingine wa shule hiyo, anasema shule yao ni ya kata, kuna vyoo vya wanafunzi kwa ajili ya kujisitiri lakini tatizo kubwa ni upatikanaji wa taulo hizo na kuwa na hofu na wasiwasi kila mara wanapoingia kwenye siku hizo.

Amina Ngasa anayesoma kwenye shule hiyo anasema shuleni hapo wamekuwa wakipewa msaada wa taulo hizo kutoka kwenye mashirika mbalimbali ya kihisani lakini zikiisha wanarudi kutumia mbinu za asili.

"Tunachokiomba kwa serikali ishushe kodi za taulo ili tuzinunue ikibidi kwa Shilingi 500 bei ambayo hata sisi tunaweza kununua kwa kujibana, kuliko hivi sasa zinauzwa Shilingi 2,000 hadi 3,000 na hatuwezi kuzimudu wakati pamoja na walezi wetu tukiwaomba hela wanasema hawana hivyo tunabakia kwenye njia za asili," anasema Amina.

Anakumbusha kuwa ni vyema zikafikishwa vijijini kwani huko ni bidhaa adimu na wasichana wengi wanazihitaji lakini hazipatikani hadi mijini.

Mwalimu wa afya wa shule hiyo, Lucia Maugo, anasema hali ya upatikanaji taulo za kike ni tatizo vijijini, hivyo wanachokifanya kwa wanafunzi ni kuendelea kutoa elimu ya hedhi salama, pamoja na mbinu za kujistiri ili wasiwe watoro wanapokuwa kwenye vipindi hivyo.

Anasema baada ya kutoa elimu hiyo ya hedhi salama, hakuna utoro wa wanafunzi licha ya kutumia vitambaa hivyo akisema zamani shuleni hapo kulikuwa na utoro wa wanafunzi wa kike kipindi wanapoingia kwenye siku zao, lakini baada ya kupewa elimu ya hedhi salama na mbinu mbadala ya kujistiri utoro unapungua.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Pandagichiza Laurent Richard, anasema mpango wa shule hiyo kujenga vyoo kwa ajili ya wanafunzi kujistiri na hedhi upo, ambapo kuna matundu ya choo yalishachimbwa kwa nguvu za wananchi, ambayo ndiyo wamepanga kutenga kuwa vyoo vitakavyotumiwa na wasichana.

Anasema kwa sasa wanafunzi shuleni hapo wanatumia vyoo vya kawaida kujistiri na hedhi, lakini wanakabiliwa na upungufu wa matundu 11 mahitaji yakiwa 31 na yaliyoko sasa ni 20 wakati idadi ya wanafunzi ni 726 kati yao wasichana wanatumia matundu 12, na wavulana nane.

Degratius Mashamba ni Mtendaji wa Kata ya Pandagichiza wilayani Shinyanga, anasema kata hiyo ina shule nne za msingi na sekondari iko moja na shule hizo za msingi zilizo na vyoo kwa ajili ya matumizi ya hedhi ni Sayu, Shilabela pamoja na sekondari, huku shule za Pandagichika na Ng'wamadelenha zikikosa vyoo hivyo.

"Mkakati wa kujenga vyoo vya hedhi upo kwenye shule hizo, ambapo tuna hamasisha

**INAENDELEA UK.12**

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Ziwe zama za kutafiti matumizi, kuandika kamusi kukuza Kiswahili

JITIHADA za kuendeleza matumizi ya Kiswahili katika nyanja tofauti za maisha na uchumi kwa jumla zinaendana na juhudi za taasisi zinazohusika na kukua kwa lugha kutoa mwanga pale ambapo kuna hitilafu katika matumizi ya lugha.

Kwa mfano kupatikana kwa neno pale ambapo hitaji lipo mathalani, 'mask' likaibuliwa neno la 'barakoa'.

Jitihada hizo za kitaasisi kujenga lugha zimewezesha maeneo mengi kupatikana kwa mifumo ya kujieleza ambayo labda ingechukua muda kujijenga yenyewe miongoni mwa watu, au isingekuwapo.

Hata hivyo mara nyingi jitihada hizo hazielekei kujaza pengo halisi ila kulijaza kwa lafudhi ya Kiswahili.

Hapo ndipo unazuka utatanishi kuhusu matumizi ya misemo tofauti kama ni Kiswahili sanifu, au ni 'Kiswahili gani na kuna baadhi ya wataalamu wa Kiswahili wameanza kukosoa baadhi ya matumizi katika lugha ya kawaida kuwa ni mifumo ya kuongea Kiingereza na haifuatani na sarufi ya Kiswahili.

Tatizo hapo ni kuwa watu wakishaanza kuwasiliana au kuzungumza kwa mfumo fulani unaoeleweka, mtu hawezi kuja kama mtaalamu akaanza kuwafundisha kitu kingine.

Inakuwa kana kwamba wanahitaji kufaulu mtihani wakati sivyo, au waongee Kiswahili kinachofurahisha wataalamu au watu fulani.

Wanafunzi wa shule za msingi na zaidi sekondari wanafahamu kitabu kinachoitwa 'Common Mistakes in English,' makosa yanayofanywa kila wakati katika kuongea Kiingereza, lakini pengine kwa Kiswahili si rahisi kuwa na kitabu kama hicho.

Yako maeneo kwa uhakika unaweza kusema kuwa ni 'common mistake,' ni kosa la kawaida linafanyika katika maongezi, halafu ziko sehemu nyingine ambako ni matumizi ya kawaida na siyo makosa ya kuainishwa kwa njia isiyopingika.

Kwa mfano katika mazungumzo redioni unasikia mwanamuziki akumbushie 'nyimbo hii' aliitunga katika mazingira gani...

Ni wazi kuwa umoja ungestahili kutumika hapo, ambao ni 'wimbo' lakini katika lugha hakuna amri au sheria ni wapi kuna majina au maneno yasiyotofautiana na wingi wake, na wapi tofauti inajitokeza.

Kwa mfano hakuna wingi kwa wanyama ng'ombe, kuku, mbuzi, kondoo au farasi inabaki tu kusema 'wengi,' badala ya kubadilisha neno. Na siyo kundi hilo tu la majina, kuna 'nyota' iwe ni moja au ziwe nyingi au anga nzima bado ni nyota.

Hivyo kuna uwezekano katika Kiswahili kuwa na mazoea ya kupuuza wingi au umoja, mradi tu neno liwe 'linatamkika,' na ndiyo huu usemi wa 'nyimbo hii' ambao sasa ni 'fashion.'

Kuna eneo jingine ambalo haliwezi kuingizwa katika usanifu ila kuonekana katika matumizi ya lugha, hata kama wasanifu wa lugha wataona kama inatumika kwa makosa, kwa maana ya hisia ya kubania 'pumzi' katika kujieleza. Dhamira hapo inakuwa ni kupunguza makali ya kitu kinachozungumziwa, au kuainisha (kuweka mkazo wa aina fulani), ingawa inaonekana kubana kujieleza kwa hisia halisi inatokea mara nyingi zaidi.

Kwa mfano ni kawaida kusema 'naomba' sukari, wakati ananunua bidhaa hiyo, na hivyo 'haombi' ila anakwepa kusema 'lete,' 'nipe' au 'nataka,' kwa sababu za ustaarabu na upole ambayo ni sawa na 'adabu' kwa Kiswahili, licha ya kuwa 'kutaka' sukari dukani siyo 'kukosa adabu.'

Halafu kuna hisia miongoni mwa 'wanazuoni' wa Kiswahili au wasanifu ambazo kimsingi hutokana na jamii inayowazunguka, si kwa maana ya jamii pana ya Watanzania ila jamii finyu kwa mfano ya wakazi wa Kariakoo, au kundi la mtaani ambako mzungumzaji au msanifu, huyo anakuwapo mara kwa mara, na hata iwe familia anakoishi.

Kwa mfano mtaalamu mmoja ambaye lafidhi anasema 'lafudhi' kwa jinsi ulimi wake ulivyokuwa unasikika redioni ni mkazi wa maeneo ambako watu wa jamii ya Kiarabu ni wengi.

Anasema 'nachukua nafasi hii' ni kosa, ingekuwa 'natumia nafasi hii' suala ambalo hakuna uhakika kama ni ukosoaji sahihi na pia anadai kuwa 'nawaambieni' siyo sahihi ila 'nakuambieni,' mwelekeo ambao pia una utata kudai hayo ni matumizi sahihi zaidi ukiwa mbele za watu.

Hapo kuna maeneo mawili ya hisia yanayokinzana, kwanza ni eneo la matumizi ya adabu ukiwa mbele za watu, ambako 'nachukua nafasi hii' ina ladha nzuri zaidi ya 'natumia nafasi hii,' na kwa upande mwingine 'nawaambieni' inakubalika kihisia, kiadabu, wakati 'nakuambieni' ina shari ndani yake. Ndiyo maana mara kadhaa baadhi ya wadadisi wanaona kuwa wasanifu wangetafiti matumizi ya lugha na mapana yake, wakaandika kamusi za vina vya matumizi ya maneno, si kupania kuwa viranja wa lugha kuondoa 'Kiingereza' katika sarufi, wakati jambo hilo linatokana na matumizi ya kawaida.

Si uelewa wa Kiingereza, ila ni kweli yako maeneo ambako Kiingereza kilisaidia kufuma ubongo wa lugha kwa jumla. Kiingereza ndiyo msingi wa lugha kwenye taalumu za teknolojia zinazotumika leo.

Yote hayo yanaonyesha kuwa watafiti wangetafiti zaidi matumizi ya lugha na mapana yake na kuandika kamusi za kina za matumizi ya maneno .

Si wakati wa kukosoa zaidi bali kuboresha na kukipa Kiswahili msamiati mpana, unaokubalika na kuchukuliwa na wengi badala ya kung'ang'ania 'nachukua nafasi hii' badala ya 'natumia nafasi hii.'

Ikumbukwe msingi wa maelezo au tungo hizo ni Kiingereza 'may I take this opportunity'...kwa kuwa ndicho kilisaidia kufuma ubongo wa lugha kwa jumla.




Watoto wanahitaji matini na vitabu vya kutosha vya Kiswahili, zaidi ya kufundishwa au kukosolewa kila wakati kwenye matumizi ya maneno. **PICHA: MTANDAO**

# Ukosefu taulo za kike bado kitendawili kinachotesa wasichana shule za vijijini

**INATOKA UK.11**

wananchi wachangie nguvu kwa kuanza kuchimba mashimo ya matundu ya choo, na kujenga hadi hatua ya renta kisha serikali ina malizia," anasema Mashamba.

Vyoo vinavyotumiwa wakati wa hedhi vina maji, pedi kwa ajili ya familia zisizo na uwezo wa kununua na ndoo za kuwekea taka za hedhi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Pandagichiza, James Sitta, anasema awali walihamasisha wananchi kuchimba mashimo ya matundu ya choo katika Shule ya Msingi Pandagichiza, lakini kwa sasa wapo kwenye msimu wa kilimo, ambapo wengi hushinda mashambani, na muda wa kiangazi ukifika ndipo wataendelea na hamasa ya ujenzi wa vyoo shuleni hapo.

Meneja Mradi wa kizazi kipya kutoka Shirika la Red Cross mkoani Shinyanga, Dismasi Kiwale, anasema katika mradi huo walikuwa wakitoa msaada wa taulo za kike kwa wanafunzi pamoja na elimu ya kujitambua, ili kupunguza utoro.

"Mradi wetu huu wa kizazi kipya ulianza mwaka 2017, lakini ulikoma Septemba 30, mwaka jana, na ulikuwa msaada mkubwa sana kwa wasichana katika kupata taulo na kuhudhuria masomo bila ya kukosa licha ya kuwa katika hedhi," anasema Kiwale.

"Mwanafunzi anapotumia njia za asili kujihifadhi, afya yake iko kwenye matatizo, hujui usafi ukoje wa kitambaa ambacho anakitumia, pia hawezi kuwa huru darasani, sababu vitu hivyo anavyotumia haviwezi kufyonza damu kikamilifu na wakati mwingine vinaweza visimsaidie kikamilifu tofauti na anapotumia pedi," anasema Kiwale.

Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto mkoani Shinyanga, Joyce Kondoro, anasema matumizi ya njia za asili wakati wa hedhi ikiwamo kuweka vitambaa kunahitaji usafi wa hali ya juu ili kuua vimelea vya magonjwa au bakteria.

Anasema, vitambaa hivyo vinahitaji kufuliwa kikamilifu na kuanikwa kwenye jua au kupigwa pasi, ili vinapotumika viwe na usalama na kutoleta madhara kwa mwanafunzi.

Baadhi ya magonjwa yanayoweza kusababishwa na ukosefu wa taulo za kike ni pamoja na maambukizi ya njia ya mkojo (UTI), fangasi, kujikuna na wakati mwingine kutokwa na uchafu sehemu za siri unaotokana na mashambulizi ya vimelea (bacteria).

"Matumizi ya njia za asili yanahitaji usafi wa hali ya juu, ili kuepusha sha fangasi kwenye njia ya uzazi, na vitambaa hivyo havitakiwi vikae ndani ya saa tano bali vibadilishwe, na siyo kukaa navyo hadi jioni,"anasema Kondoro.

"Mwanafunzi anapokuwa akitumia vitambaa au njia nyingine kutokana na umri wao hawako salama, kuna uwezekano wa kupata maambukizi kwenye mfumo wa uzazi, tofauti na pale wanapokuwa wamevaa taulo za kike, ambazo zenyewe ni salama kwao na zitawafanya wasome kwa kujiamini," anaongeza.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Siri Jiji Dar kutakata mtihani la saba 2021

## ■ Mkurugenzi atoboa ushindi ulivyopatikana



Mazingira bora pamoja na miundombinu wezeshi ya kujifunza na kufundishia ni sehemu ya mafanikio ya elimu mkoani Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

MKOA wa Dar es Salaam umeongoza kwenye matokeo ya darasa la saba kitaifa mwaka 2021 na kuwa kinara Tanzania Bara.

Akitangaza matokeo hayo Oktoba 2021, Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), Dk. Charles Msonde, anasema Wilaya ya Kielimu Ilala Mjini, inaongoza kwa ufaulu ikibeba asilimia 98.52. Ikimaanisha kuwa kwa kila wanafunzi 100 waliofanya mtihani karibu 99 walifaulu.

Licha ya kufuatiwa na Halmashauri ya Jiji la Arusha yenye asilimia 98.50, kutoka Dar es Salaam, Wilaya ya Kinondoni ni ya tatu ikibeba asilimia 98.35 za ufaulu, Manispaa ya Kigamboni Dar es Salaam, imeshika nafasi ya tisa wakati Wilaya ya Kielimu Ilala Vijijini ni ya 10 kwa kupata asilimia 96.28.

Dk. Msonde anasema Dar es Salaam imeongoza kitaifa kwa asilimia 96.54 ikifuatiwa na Iringa iliyofikisha asilimia 91.01, na Mbeya ni ya tatu kwa asilimia 88.14.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Jumanne Shauri, anataja baadhi ya mbinu zilizoleta ushindi kuwa ni kushirikiana na ushirikishwaji wa wadau kuanzia wanafunzi, wazazi, walezi, viongozi wa mitaa, kata na jiji.

Aidha, ufuatiliaji wa mara kwa mara shuleni wa changamoto za wanafunzi na walimu na kuzitatua vyote vimeinua ufaulu.

Anataja fedha UVIKO-19 zilizotolewa na serikali kuboresha elimu ziliongeza vyumba vya madarasa msingi na sekondari na pia mapato ya ndani ya halmashauri yaliyoelekezwa kwenye elimu, vimeongeza ufanisi.

### MATOKEO 2021

Shauri anasema waliofanya mtihani wa kuhitimu darasa la saba mwaka jana Wilaya ya Ilala inayounda Jiji la Dar es Salaam ni 27,775 wakati Wilaya ya Kielimu ya Ilala Mjini walikuwa 13,852.

Kati yao wavulana walikuwa 6,820 na wasichana 7,103 na kushika nafasi ya kwanza kitaifa.

Änasema Wilaya ya Kielimu Ilala Vijijini, walikuwa 13,852, wavulana 6,724 na 7,128, ni wasichana, wakishika nafasi ya 10 kitaifa.

“Ufaulu huo umeongezeka kwa asilimia nne ikilinganishwa na mwaka jana 2020, ambao wanafunzi waliofanya mtihani wa darasa la saba walikuwa 28,269, wavulana 13,813 na wasichana ni 14,456. Waliofaulu walikuwa 26,447, huku wavulana wakiwa 12,889 na wasichana 13,558,” anasema Shauri.

Hadi mwaka jana Dar es Salaam ilikuwa na shule za msingi 254 za serikali ni 127 na za binafsi ni 127, zenye wanafunzi 224,327, kati ya hao 215,302 ni wa shule za msingi, na waliobakia 9,025 wako shule ya awali. Kwenye shule za msingi, wavulana wapo 106,721 na wasichana ni 108,581, darasa la awali likiwa na wavulana 4,646 na wasichana 4,379.

### MBINU ZA USHINDI

Shauri anazitaja kuwa ni mikutano ya wadau wa elimu kusikiliza mawazo ya kujenga, kupata changamoto za walimu, kuwapa uzoefu watahiniwa wa sekondari kwa kuwafanyisha mitihani ya pamoja na kwamba hilo limefanikiwa kwa kiasi kikubwa.

“Mikutano ya wadau inawapa walimu fursa ya kueleza changamoto za mazingira ya kazi, ambazo hupatiwa ufumbuzi. Kazi zinafanywa kwa ushirikiano na wazazi, walezi, viongozi wa mitaa, kata, walimu na viongozi kwenye halmashauri,” anasema Shauri.

Aidha, Shauri anasema baadhi ya shule za msingi zimeongezewa madarasa na vyoo kwa kutumia mapato ya ndani na kwamba kuanzia Julai hadi Desemba 2021 madarasa 47 yamejengwa kila moja likigharamu Sh. milioni 15.

Aidha, vyoo 17 vimejengwa kila tundu likitumia milioni 1.1, madawati 67 yamechongwa kwa gharama ya 150,000 kila moja.

### FEDHA ZA UVIKO

Anasema Shule ya Msingi Kivule na Yongwe iliyoko Chanika, kila moja imepata Sh. milioni 11,872,379 kwa ajili ya kuweka tangi na gata za kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya kunywa na kujenga eneo la kunawia mikono.

Akizungumzia sekondari, anasema zimetengwa Sh. bilioni nne za mapato ya ndani na tayari shilingi bilioni 1.02 zimeshatolewa kwa ajili ya vyumba vya madarasa 102.

Aidha, shule za Kipunguni, Kiwalani, Minazi Mirefu, Mivinjeni, Amani (Ukonga), Buguruni, Bonyokwa na Vingunguti, zitajengewa madarasa ya ghorofa.

Aidha, Jiji limepata Shilingi bilioni 5.1 za UVIKO -19 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 255 katika shule 41 za sekondari. Kadhalika Shauri anasema Halmashauri ya Jiji itajenga vyoo kwa gharama ya Sh. milioni 222 kwenye shule 14 na mabweni mawili yenye thamani ya Sh. milioni 240 katika shule maalum ya Michezo Mvuti, iliyoko kata ya Msongola.

Kwa mujibu wa Shauri, Dar ina sekondari 108, za serikali ni 60 na binafsi 48, vyumba vya madarasa 1,021 lakini mahitaji ni 1,627 kukiwa na upungufu wa vyumba 606. Vyoo vipo 1,222, wakati mahitaji ni 1,468 hivyo pungufu ni 246.

Nyumba za walimu zilizoko ni 83, mahitaji 2,192, upungufu ni 2,109 na ina walimu 2,192 wakati mahitaji ni walimu 2,924.

Katika kupambana na utoro, wameimarisha bodi za shule na kushirikisha Polisi Jamii kwenye kata za Msongola, Chanika na Buyuni zilizoko pembezoni ambazo mtoto anaweza kujificha.

### MALENGO ELIMU MSINGI

Anasema kuongeza uandikishaji kwa kuzingatia fursa sawa, kuinua ubora wa elimu ngazi zote, kusimamia uwezo wa utendaji kazi, kushughulikia masuala ya mtambuka, kuimarisha taratibu za kitaasisi, kufanya utafiti, ufuatiliaji na tathmini za kielimu.

Kupunguza idadi ya watu wazima mbumbumbu, kuinua ubora wa mazingira ya kufundishia na kujifunza, kuongeza idadi ya madarasa na watoto wa shule za awali, kuhakikisha kuwa elimu ya UKIMWI na VVU, inatolewa, mazingira na stadi za maisha zinafundishwa kwa ufanisi katika shule za msingi na kusimamia upatikanaji na uwezeshaji wa mazingira kwa wanafunzi wenye ulemavu.

Diwani wa Kata ya Mzinga, Job Isaac, akitoa maoni yake anasema kata yake, inajenga sekondari mpya ya Magole, kumalizia vyumba vitano vya madarasa kwa kutumia mapato ya ndani, kadhalika fedha za UVIKO-19 zimejenga madarasa 12.

“Shule za msingi Magole na Mafanikio zote zina madarasa mawili kila moja, na ujenzi upo katika hatua mbalimbali, shule ya Msingi Mzinga B, ujenzi madarasa manne unaendelea na yote yanajengwa na mapato ya ndani,” anasema Isaac.

TEKNOLOJIA

NA MARY GEOFREY

# Waziri Nape katika mazingira mapya sekta ya mawasiliano

• Ada masafa zafutwa, TV za kulipia ruksa



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnaye. **PICHA: MTANDAO**

WIZARA ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), wameboresha kanuni za miundombinu ya utangazaji dijiti na za leseni, lengo likiwa ni kuweka mazingira bora ya utoaji huduma za mawasiliano kwa Watanzania.

Na pia kuwa na uwekezaji na utoaji huduma bora pamoja na kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya kielektroniki nchini.

Maboresho ya msingi yaliyofanywa ni kwenye kanuni mbili ambazo ni za leseni na za miundombinu ya utangazaji dijiti zote za mwaka 2018. Lengo la mabadiliko haya ni kuendana na mabadiliko ya kasi ya ukuaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnaye, akidadavua maboresho hayo anasema, sehemu ya kwanza ni katika kanuni za mawasiliano ya kielektroniki na posta ya 2022.

Anasema maboresho yaliyofanyika ni pamoja na kufuta ada ya masafa kwa wenye miundombinu ya utangazaji wa televisheni dijiti (MUX) ili kuleta nafuu kwa wawekezaji kwenye eneo hili na kuwawezesha kupanua wigo wa huduma za mawasiliano pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora .

Aidha, ni kuainisha aina mpya ya leseni maalum kwa watoa huduma wanaotengeneza bando za maudhui.

"Ili kurahisisha utoaji wa leseni na pia kuhimiza watengenezaji wa maudhui wa ndani kuandaa maudhui yanayohamasisha ukuaji wa utamaduni wa Kitanzania na jamii inayoizunguka," anasisitiza waziri huyo.

Anasema pia ni kuongeza ajira kwa vijana wanaovutiwa na uandaaji wa maudhui kwa kuzingatia kuwa hitaji la soko katika miaka ya hivi karibuni limeongezeka kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ongezeko la idadi ya watu.

Jambo jingine ni kubadili leseni ya vituo vya utangazaji vya kijamii kuwa leseni ndogo kwa lengo la kuchochea uanzishwaji wa vituo vya utangazaji vya kijamii kwenye maeneo yasiyofikiwa au yanayopata huduma hafifu za utangazaji hasa wa redio.

"Hatua hii pia itawezesha wananchi kunufaika kwa kupata huduma za maudhui ya utangazaji yanayoakisi maisha na tamaduni zao katika maeneo husika," anasema.

Anaeleza zaidi kuwa, upatikanaji wa leseni hizo utachukua muda mchache zaidi kwa kuwa mlolongo wa uchakataji wa leseni umefupishwa tofauti na leseni kubwa ambazo zinahitaji mchakato wenye mlolongo zaidi hadi hatua ya mwisho ya ukamilishwaji.

Nape anasema jambo la nne ni kupunguza ada za leseni ili kuwezesha utoaji huduma nafuu na wenye viwango utakaosaidia kukuza ajira na kuvutia watu wengi zaidi kuwekeza katika sekta ya Mawasiliano nchini.

Jingine kwa mujibu wa waziri ni kuainisha aina mpya ya leseni ya utangazaji kwa maudhui maalum ya elimu ili kutoa nafasi kwa taasisi au mashirika yanayonuia kutoa huduma ya elimu kwa kuzingatia kwamba mazingira ya ambayo yamekuwa yakibadilika katika miaka ya karibuni kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo mlipuko wa maradhi kama vile UVIKO-19 ulichagiza kubadilika kwa modali ya uwasilishaji elimu maeneo mengi duniani ikiwamo Tanzania.

Anasema maboresho katika Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Redio na Televisheni), 2021 maboresho yaliyofanyika kwenye kanuni zinazoongoza huduma za utangazaji wa televisheni na redioni kuruhusu chaneli za televisheni za kulipia na kuchukua matangazo ya kibiashara (yasiyozidi dakika tano kwa saa).

"Kabla ya maboresho haya ya kanuni, haikuruhusiwa chaneli za televisheni za kulipia kuweka matangazo ya kibiashara," anaeleza Nape.

Jambo jingine anasema ni kuruhusu chaneli za televisheni za kutazamwa bila kulipia (free to air) zionyeshwe bila kulipia katika visimbuzi vyote nchini pasipo kujali ni vya kulipia au la.

Kabla ya maboresho haya ya kanuni, chaneli za kutazamwa bila kulipia hazikuruhusiwa kuonyeshwa katika ving'amuzi vya kulipia nchini.

"Lengo la maboresho katika eneo hili ni kuongeza wigo wa mapato kwa watoa huduma wa chaneli za kutazamwa bila kulipia; kuongeza wigo wa ufikiwaji wa habari kwa wananchi kwa sababu kwa maboresho haya kila king'amuzi kitaweza kuonyesha chaneli zote, za kulipia na zisizo za kulipia," anasisitiza.

Anafafanua zaidi kuwa, hatua ya kuruhusu visimbuzi vyote kubeba chaneli za bila kulipia kunaongeza na kuwezesha uhuru wa watazamaji kuchagua chaneli watakazo kirahisi; pia itawezesha kutatua changamoto ya mtumiaji kulazimika kumiliki kisimbuzi zaidi ya kimoja.

Sehemu nyingine iliyofanyiwa kazi na serikali ni maboresho katika kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Simu na Intaneti) ya mwaka 2021 na mambo kadhaa yamefanyiwa maboresho na marekebisho.

Mkuu wa Kitengo cha Ufuatiliaji wa TCRA, Philip Filikunjombe, anasema wanalenga kuboresha mfumo wa leseni kwa kuainisha leseni ya vituo vya kuhifadhi taarifa (public data centre license).

Anasema maboresho hayo yanalenga kuongeza wigo wa uwekezaji katika huduma za mawasiliano hasa katika masuala ya kuhifadhi taarifa kutokana na ongezeko la huduma mtandao.

Filikunjombe anasema kuainisha leseni kwa ajili ya vituo vya maingiliano ya mtandao (internet exchange points).

Anafafanua kuwa, maboresho hayo yatawezesha kuainisha vigezo vya kiufundi vya miundombinu ya vituo vya maingiliano ya mtandao.

Anataja eneo jingine kuwa ni kupunguza ada za masafa ya mawasiliano ya redio ili kuhimiza upelekaji wa mtandao (network expansion) katika maeneo mengi zaidi nchini.

Anaeleza kuwa, mabadiliko hayo yanaendana na Dira ya Maendeleo ya 2025 inayolenga kuhakikisha ufikishwaji wa huduma za TEHAMA kwa wananchi wote.

Filikunjombe anasema maboresho ya nne yanahusisha kupunguza ada ya vituo vya mawasiliano ya redio kutoka dola 3,000 na kuwa dola 100 kwa kituo, ili kuongeza kasi ya usambazaji wa intaneti yenye kasi nchini hasa maeneo yasiyofikiwa kirahisi na miundombinu iliyopo.

Aidha, anasema ni kuainisha ada kwa ajili ya mawasiliano ya simu kwa njia ya setilaiti ili kuongeza udhibiti wa huduma za mawasiliano ya simu kwa njia ya setilaiti.

Anasema hatua ya kuondoa ada ya usajili kwa madishi ya mawasiliano ya redio ili kuongeza usambazaji wa huduma.

Aidha, wamepunguza ada za madishi ya mawasiliano ya redio (VSAT) kutoka dola 3,000 na kuwa dola 60 ili kuhimiza matumizi ya VSAT na pia kuchochea uwekezaji kwenye eneo hili.

Anasema pia kutofautisha kati ya leseni ya kutengeneza vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki kwa mafundi wakubwa na wadogo.

Mabadiliko ya tisa anasema yanahusu kupunguza ada mbalimbali za leseni ili kupunguza mzigo wa ada kwa watoa huduma na kuhimiza uwekezaji zaidi na mwisho kuongeza aina mpya ya leseni ndogo kwa ajili ya huduma mtandao.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano TCRA, Semu Mwakianjala, anasema maboresho ya kanuni ni suala muhimu katika kuhakikisha utoaji wa huduma za mawasiliano unaendana na mabadiliko ya teknolojia na uhalisia wa mazingira yaliyoko.

Anasema dhamira ya serikali ni kuendelea kufanya maboresho ya Kanuni kila itakapohitajika kwa kuzingatia kuwa teknolojia inabadilika kila mara kama mkondo wa maji unavyobadili njia zake kila mtiririko unavyosonga.



## SIDO yapewa mbinu uanzishwaji viwanda vingi mijini na vijijini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira imelitaka Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) kuongeza ubunifu wa kutafuta njia mbalimbali za kutunisha mtaji wa Mfuko wa Taifa Kuendeleza Wajasiriamali Wananchi (NEDF) ili wananchi wengi mijini na vijijini waanzishe viwanda vidogo vidogo.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Erick Shigongo, aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye kikao cha kupokea taarifa ya utekelezaji wa mfuko huo.

Alipongeza jitihada zinazofanywa kuimarisha mfuko huo na kutaka kuongezwa kwa njia hizo ili kuwa na mtaji mkubwa, utoaji wa mikopo mijini na vijijini kwa kuzingatia makundi maalumu, muundo wa uendeshaji, viwango vya mikopo, vigezo vya kupata mikopo, riba ya mikopo hiyo na ufadhili wa vikundi vya wajasiriamali.

Naye Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, aliihakikishia kamati hiyo kuwa wizara itayafanyia kazi maoni na mapendekezo yaliyotolewa ili kuhakikisha SIDO inaongezewa mtaji katika mfuko wa NEDF na kuongeza kasi ya uanzishaji na ukuzaji wa viwanda vidogo nchini ambavyo vitaongeza ajira na kukuza biashara na uchumi wa nchi.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Exaud Kigahe, alisema ni muhimu kuiwezesha SIDO kuongeza mtaji katika mfuko huo wa NEDF kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya fedha ikiwamo kishirikiana na taasisi za umma ili mfuko huo usaidie wananchi wengi wanaohitaji mitaji ya kuanzisha viwanda vidogo vya kuzalisha bidhaa mbalimbali.

Awali, akitoa utoaji wa taarifa ya utekelezaji wa mfuko, Mkurugenzi Mkuu wa SIDO, Mhandisi Prof. Sylvester Mpanduji, alieleza kuwa mfuko huo umedumu tangu kuanzishwa kwake mwaka 1994.

"Huu mfuko umepokea jumla ya Sh.bilioni 6.64 katika kipindi cha mwaka 1994/95 hadi 2020/21 kama mtaji na kuukuza hadi kufikia Sh. bilioni 9.76.

Aidha, Prof. Mpanduji alisema huduma za kifedha za mfuko wa NEDF zimeendelea kutolewa katika mikoa yote na inajipanga kutoa huduma hiyo katika kila wilaya huku ikitafuta njia bora za kuimarisha mfuko na kukusanya madeni sugu ya mikopo iliyotolewa.

# NGO 6,147 zatajwa kutekeleza majukumu kwa mujibu wa sheria

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) 6,147 kati ya 11,946 yaliyosajiliwa ndiyo yanatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria na kanuni.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, aliyasema hayo juzi alipokuwa akitoa taarifa ya usimamizi, utekelezaji, mafanikio na kero za mashirika hayo kwa kipindi cha 2019/2021 mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Maendeleo ya Jamii jijini hapo.

Alisema mashirika hayo 11,946 yaliyosajiliwa kuanzia mwaka 2005 hadi Januari, 2022 na zaidi ya 6,000 hayajulikani yaliko.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya Bunge, Aloyce Kamamba, alisema hakuna sababu ya kuwa na orodha kubwa ya mashirika hayo wakati yanayofanya kazi kwa mujibu wa sheria ni machache.

Aidha, alipongeza jitihada zinazofanywa na wizara katika kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa NGO's na kusisitiza kuboresha mikakati iliyoko. Katika hatua nyingine, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula, aliyataka mashirika hayo kufanya kazi ya kuhudumia jamii kulingana na katiba zao, mikataba na vibali vya kutekeleza miradi kama ilivyoidhinishwa na msajili wa NGO.

Akizungumza na wawakilishi wa mashirika hayo kutoka mikoa ya Dodoma, Iringa, na Singida, Dk. Chaula alisema pamoja na mashirika hayo kuchangia maendeleo ya taifa ni vema uwajibikaji wake ukazingatia misingi iliyowekwa.

Alimtaka Mwenyekiti wa Baraza la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) kuhakikisha mashirika 170 ambayo yamesajiliwa mkoani Dodoma na hayafanyi kazi ambayo ni sawa na asilimia 47 ya mashirika 358 yatafutwe ili kujua yanafanya nini.

Mwenyekiti wa NaCoNGO, Dk. Lilian Badi, alimhakikishia Katibu Mkuu kufanya kazi kwa ushirikiano na kufuata sheria, taratibu, kanuni na miongozo ya uendeshaji wa mashirika hapa nchini.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, akizungumza na wanafunzi kutoka shule mbalimbali na wananchi walioshiriki upandaji miti Medeli jijini Dodoma jana, ikiwa ni Wiki ya Uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021, inayotarajiwa kuzinduliwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango Februari 12. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jaji aipa neno Tume ya Utumishi ya Majeshi

**Na Renatha Msungu** DODOMA

JAJI Mfawidhi wa Mahakama Kuu, Kanda ya Dodoma, Gerson Mdemu, amewataka wajumbe wa Tume ya Utumishi ya Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Uhamiaji kuhakikisha wanaisoma na kuielewa sheria inayosimamia majukumu ya chombo hicho.

Jaji Mdemu alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki jijini hapa baada ya kuwaapisha wajumbe wa tume hiyo.

Alisema watumishi wa Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Uhamiaji ni vema wakapewa elimu kuhusu sheria na taratibu ili utekelezaji wa majukumu ya tume hiyo yafanyike vizuri na kuepuka kwenda nje kutafuta suluhu.

"Elimu hii ya majukumu ya tume isiishie kwa viongozi na wakuu wa vyombo ambavyo viko ndani ya tume, bali iende kwa watumishi ambao wanawajibika kwenye tume, kwani wao ndio wanaojua taratibu za nidhamu wanazotakiwa kuzingatia ili waweze kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu,"alisisitiza.

Alisema kila mmoja anapaswa kujua wajibu wake katika kazi ambazo wanafanya ni si kwenda kinyume na sheria ya kazi yao.

Mwenyekiti wa Tume hiyo ambaye ni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alimhakikishia Jaji Mfawidhi huyo kuwa wajumbe watahakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa uadilifu na weledi wa juu kwa ajili ya maendeleo ya vyombo vinavyosimamiwa tume na taifa kwa ujumla.

Alisema hakuna atakayefanya kazi kinyume na sheria, isipokuwa wote watafuata walichoagizwa kufanya ili kutekeleza majukumu yao.

Alieleza lengo lao ni kuona sekta hiyo inakuwa mstari wa mbele kusimamia haki za wananchi kwa weledi.



# H'shauri yaanzisha duka la dawa kuondoa ukiritimba

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, imeanza mchakato wa kuanzisha duka la dawa ambalo litakuwa linatoa huduma kwa wananchi wote wa wilaya hiyo, lengo likiwa ni kupunguza gharama za ununuzi wa dawa kama ilivyo sasa.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Katule Kingamkono kwenye vikao vya Baraza la Madiwani, waliazimia kuanzisha duka kubwa la dawa ambalo litahudumia wakazi wa Kyela na nje.

Alisema duka hilo litapunguza usumbufu wa kwenda kununua dawa maeneo ya mbali, kwamba wakati mwingine huuziwa kwa gharama kubwa.

"Tumeona tatizo la upatikanaji wa dawa za binadamu katika Wilaya ya Kyela. Wagonjwa wanaokwenda kutibiwa Hospitali ya Wilaya wamekuwa wakilalamika pindi dawa zinapokosekana. Wanalazimika kununua kwenye maduka ya watu binafsi," alisema Kingamkono.

Aliongeza kuwa duka hilo litasaidia kuondoa ukiritimba unaofanywa na baadhi ya watumishi ambao aidha wana maduka yao ya dawa kwa sababu ya maslahi binafsi.

Kingamkono alisema duka hilo litakuwa mwarobaini wa kutatua vikwazo vyote walivyokuwa wakipata wagonjwa wanaotibiwa hospitali ya wilaya na kwamba litakuwa linatoa huduma ndani ya hospitali hiyo.

Diwani wa Viti Maalum, Tumain Mwakatika alisema duka hilo litasaidia kinamama wajawazito kupata matibabu kwa wakati kuliko ilivyo sasa kwamba wanapokosa dawa hulazimika kuzifuata nje ya hospitali hiyo.

Alisema dawa za nje ya hospitali zinauzwa kwa gharama kubwa ukilinganisha na bei elekezi ya serikali na kwamba mchakato wa kujenga duka kubwa la dawa ambalo litamilikiwa na halmashauri ili lianze kutoa huduma.

Aidha, alieleza kuwa duka hilo litakuwa ni miongoni mwa chanzo cha mapato ndani ya halmashauri hivyo fedha zitakazopatikana zitasaidia kujenga miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema katika bajeti ya mwaka 2021/2022 kwa pamoja wamepitisha ujenzi wa duka kubwa la dawa ambalo litakuwa ndani ya Hospitali ya Wilaya.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Momba mkoani Songwe, Twaha Masoud, akichangia damu katika maadhimisho ya kuzaliwa kwa chama hicho, yaliyofanyika Kata ya Kamsamba hivi karibuni. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Maofisa ugani wapewa pikipiki kuwafikia wakulima

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, imekabidhi pikipiki 13 zenye thamani ya Sh. milioni 32 kwa maofisa wa kilimo.

Lengo la kukabidhi pikipiki hizo ni kurahisisha katika shughuli zao za kuwapatia elimu na mbinu wakulima wilayani humo.

Akikabidhi pikipiki hizo juzi, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Twalibu Lubandamo aliwataka maofisa kilimo kutumia usafiri huo kuzitumia kwa malengo yaliyokusudiwa ambayo ni kuwasaidia wakulima kujinufaisha na kilimo.

Alisema pikipiki hizo zitasaidia kuwafikia wakulima wa maeneo ya pembezoni ambayo kwa kiasi kikubwa yalikuwa hayafikiwa kutokana na tatizo la miundombinu ya barabara.

"Wananchi wa Wilaya ya Mbarali wengi wao wanajihusisha na kilimo, tunawategemea maofisa wetu mtakwenda kutanua wigo katika uzalishaji wa mazao, watembeleeni wakulima waliopo kata kwa kata, vijiji na vitongoji muwapatie mafunzo ya uzalishaji wenye tija ili waendelee kunuifaika na kilimo," alisema Lubandamo.

Akizungumzia utolewaji wa pikipiki hizo, Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Missana Kwangura, alisema kwa kushirikiana na idara ya kilimo wataendelea kutenga bajeti ya kuwawezesha usafiri maofisa ugani kila mwaka.

Alisema lengo la kutenga bajeti hiyo ni kuwawezesha usafiri maofisa ugani kuyafikia maeneo yote ya wakulima na kuchangia kuinua mapato ya halmashauri kupitia kilimo ambacho kinachangia kwa kiasi kikubwa mapato ya halmashauri hiyo. Kwa upande wake, Ofisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wa wilaya hiyo, Daniel Kamwela alisema pikipiki hizo zitahudumu ndani ya kata 13 na kwamba katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 waliwawezesha maofisa ugani pikipiki nne.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2022/2023 wametenga Sh. milioni 25 kwa ajili ya kununua pikipiki kwa kata zilizobakia na baada ya hapo watavifikia vijiji vingine vinavyofanya kazi kwenye mazingira magumu.

# EWURA yataka ujenzi vituo vya mafuta kuwa na vibali

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imezishauri halmashauri na wilaya za Mkoa wa Mbeya kuangalia namna bora ya kushirikiana na mamlaka hiyo pamoja na wadau wengine katika kuhakikisha ujenzi wa vituo vya mafuta unakuwa na vibali husika.

Akizungumza na Nipashe, Meneja wa Kanda wa EWURA, Karim Ally, alisema mamlaka zinazohusika na utoaji wa vibali vya ujenzi wa vituo vya mafuta ni pamoja na Baraza la Usimamizi wa Mazingira NEMC , wilaya na halmashauri ambao ndiyo wanatoa hati ya umiliki wa ardhi kabla ya ujenzi kutekelezwa.

"Miongoni mwa majukumu ya EWURA ni kukagua vituo vya mafuta ambapo hadi kufikia Desemba 2021 ukaguzi wa kawaida umefanyika katika vituo 14, ukaguzi wa kiufundi katika miundombinu umefanyika kwenye vituo 15," alisema na kuongeza:

"Ukaguzi wa ubora wa mafuta umefanyika katika vituo vinne na vituo 21 vilivyopewa leseni katika kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Desemba 2021 kwa Mkoa wa Mbeya," alisema.

Ally alisema miongoni mwa vikwazo vinavyoikabili sekta ya maji ni uzalishaji mdogo katika mamlaka zinazosimamia bidhaa hiyo, ukilinganisha na mahitaji halisi kwa maeneo mbalimbali.

Alisema kipindi cha kiangazi kunakuwa na tatizo kubwa la maji kwa madai kuwa wakati mwingine baadhi ya mamlaka kukosa wafanyakazi wa kutosha ili kutoa huduma.

"Ewura pia inashughulikia malalamiko yanayohusiana na sekta zote tunazozidhibiti, miongoni mwa malalamiko ni bili za maji, kuuziwa mafuta yasio na ubora, malalamiko mbalimbali ya umeme, malalamiko ya bei za bidhaa na malalamiko ya utoaji huduma," alisema Ally.

Alisema EWURA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini katika kipindi cha Julai 2021 hadi Desemba 2021 ilipokea malalamiko 17 kati ya malalamiko hayo nane ni yale yanayotoka Mkoa wa Mbeya, malalamiko saba ni ya umeme na lalamiko moja ni la kuhusu maji.

Akizungumzia hali ya upatikanaji wa huduma za umeme, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mwalingo Kisemba, alisema hali ya upatikanaji wa umeme hairidhishi.

Alisema kwa mamlaka waliyonayo EWURA wanapaswa kuzisimamia mamlaka zote za nishati ili huduma ya umeme ipatikane kwa uhakika kuliko ilivyo sasa.





# 'Zanzibar inaweza kuzalisha sukari ya kujitosheleza'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, amesema Zanzibar inaweza kuzalisha sukari itakayotosheleza mahitaji na kupunguza uagizaji bidhaa hiyo.

Alisema hayo yatafanikiwa endapo wananchi watahamasika kulima kilimo cha miwa kwa kiwango kikubwa.

Akizungumza na waandishi wa habari Mjini Zanzibar, waziri huyo alisema kuwa kiwanda cha sukari kilichoko Mahonda kina uwezo wa kuzalisha sukari kwa wingi endapo kitakuwa na miwa ya kutosha.

Alisema miongoni mwa sababu zilizopelekea kiwanda hicho kuzalisha sukari kiwango kidogo ni uhaba wa miwa unaotokana na udogo wa eneo lao la kulima hali iliyopelekea kutoa fursa hiyo kwa wananchi na baadaye kuuza kwa kiwanda hicho.

Aidha, alisema wizara yake itaendelea kusimamia bei ya biashara ili kuendelea kuwafanya wananchi kumudu na kuhimili ukali wa maisha unaotokana na kupanda kwa bei za bidhaa.

"Baadhi ya bidhaa zimekuwa zikiongezeka bei, na Rais Dk. Mwinyi, alizitolea ufafanuzi vizuri na mipango ya serikali ya kuhakikisha wanadhibiti zaidi bidhaa walizozitolea bei elekezi," alisema.

Akizungumzia kuhusiana na suala la leseni za biashara, alisema kuwa tayari baraza la usimamizi wa mfumo wa utoaji leseni Zanzibar wamekamilisha mfumo wa taarifa za leseni kwa kuunganisha utowaji wa taarifa za kibiashara na uombaji wa leseni.

**Alisema hayo yatafanikiwa endapo wananchi watahamasika kulima kilimo cha miwa kwa kiwango kikubwa**

# Waziri ataka usimamizi wa maadili kwenye jamii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais (Fedha na Mipango), Jamal Kassim Ali, amesema ni muda mwafaka wa kusimamia maadili mema ili kuepukana na vitendo viovu katika jamii.

Akizungumza kwa niaba yake, Mkurugenzi wa Utumishi na Uendeshaji wa Wizara hiyo, Suleiman Mohamed Rashid, wakati wa sherehe za kumaliza mafunzo kwa walimu wanaofundisha madrasa ya Qur-an katika Chuo cha Kiislamu (CCK) Mazizini Mjini Unguja, alisema katika jamii kumekuwa na vitendo vingi ambavyo haviendani na maadili ya nchi kutokana na kuacha maadili mema pamoja na tamaduni, huku akiwakumbusha wahitimu hao wajibu wao kwa kuhakikisha wanazalisha jamii yenye misingi ya maadili mema.

Alifafanua kuwa misingi ya maadili mema itazalisha viongozi na watendaji waadilifu na wenye kujali wajibu wao wa kutimiza majukumu kama inavyoelezwa katika vitabu vya dini.

Naye Mkurugenzi (ukaguzi wa elimu), Maimuna Fadhili Abassi, aliwataka wahitimu hao kutotosheka na elimu hiyo bali watumie fursa mbalimbali kuongeza taaluma zao.

Kwa upande wake mwakilishi kutoka Ofisi ya Mufti Zanzibar, Othman Mohamed, aliipongeza Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Chuo cha Kiislamu Zanzibar kwa kuhakikisha wanatumia mbinu mbalimbali ili kuhakikisha jamii inarudi katika mustakabali mwema unaoendana na maadili ya dini.

Mkuu wa CCK, Bakari Chumu Ame, aliwashauri wahitimu hao kutumia taaluma waliopatiwa kuondoa mambo ambayo ni kinyume cha maadili ya kiislamu na kuifanya jamii iwe katika mustakabali mwema.

Akisoma risala kwa niaba ya wahitimu hao, Saleh Mohammed Omar aliipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa kushirikiana na Ofisi ya Mufti kwa kuandaa mafunzo hayo ili kuhakikisha jamii inapata taaluma bora ya maadili.

Alisema kutokana na kuwa mwalimu ndio kioo cha jamii, hivyo ipo haja ya walimu wa madrasa nao kuwapa taaluma hasa ya saikolojia ili kupambana na athari mbalimbali za mmong'onyoko wa maadili zinazokuwapo katika jamii.

Pia aliuomba uongozi wa chuo kuwapatia taaluma ya lugha za alama ili kuwafundisha watoto wenye mahitaji maalum ili kwa kuwa nao wana haki ya kupata elimu.



Mkurugenzi wa Utumishi na Uendeshaji wa Wizara ya Fedha na Mipango, Suleiman Mohamed Rashid (kulia), akimkabidhi cheti mhitimu wa mafunzo ya ualimu wa Madrasa za Qur-an, Saleh Muhammed Omar, katika mahafali iliyofanyika Chuo cha Kiislamu (CCK) Mazizini Mjini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Fursa nyingine ya utalii yapatikana Tumbatu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

IDARA ya uhifadhi ya maeneo ya bahari Zanzibar imeandaa utaratibu maalumu wa kufikia makubaliano na wakazi wa Kisiwa cha Tumbatu wa kuliweka katika uhifadhi wa bahari eneo la kisiwa cha Mwana wa Mwana kiliochoko ndani ya eneo la Kisiwa cha Tumbatu.

Mkurugezi wa idara hiyo, Dk. Makame Omar Makame iliyoko Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi aliyasema hayo alipokutana na uongozi wa shehia nne za Tumbatu ikiwa ni hatua ya mazungumzo na upimaji wa eneo hilo katika ofisi ya Wilaya Ndogo Tumbatu.

Dk. Makame alisema makubaliano hayo yamefikia katika hatua nzuri ambayo yanategemewa yataleta manufaa kwa kizazi cha sasa na baadaye.

Alisema hatua itakayofuata ni makubaliano ya mwisho na hatua za kuweka maboya kwa eneo lililotengwa kwa ajili ya uhifadhi huo.

Alisema katika uhifadhi huo wanategemea kutenga eneo la mita 300 ambazo hazitotumika kwa shughuli za uvuvi kwa lengo la kuvutia wageni na kuhifadhi rasilimali za bahari.

Eneo hilo la uhifadhi litatumika kwa shughuli za kiutalii kwa watalii wa ndani na nje na litatoa nafasi kwa kuwahifadhi kasa walioko katika eneo hilo ili wasiendelee kutoweka.

Dk. Makame alifafanua kuwa shughuli zitazofanyika hapo ni pamoja na kuingia kwa wageni kwa ajili ya kuzamia na kuhifadhia mayai ya kasa katika kisiwa hicho.

Alisema kufanikiwa kwa uhifadhi wa eneo hilo kutaleta fursa kwa wazawa katika kuzilinda rasilimali zilizoko na kuwanufaisha wenyeji wa maeneo ya Tumbatu.

Kisiwa cha Mwana wa Mwana kipo katika Wilaya Ndogo ya Tumbatu na ni kisiwa maarufu ambacho kimebarikiwa kuwa na vivutio vya utalii kama pomboo, kasa na mazalia ya samaki (matumbawe).

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BRIGITTE CALIST ASSENGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MERCEDES BENZ** yenye namba za usajili **T 960 CSP** chasis namba **WDC1641222A089154**, engine namba **64294040106821,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/URA/RB/53809/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DORIS GERVAS MALOLE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.12335/0009/2013 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitita shule ya secondary ya **WAZO HILL SECONDARY SCHOOL mwaka 2013, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa CD/IR/RB/12309/2016**

## YADI INAPANGISHWA-TABATA

YADI INAPANGISHWA IKO TABATA BIMA KARIBU NA SHULE YA ST.MARY'S PRIMARY NA CHUO CHA UALIMU CHA ST.MARY'S, INA UKUBWA WA SQM 3105 BEI NI MAELEWANO,YADI IKO MITA 60 KUTOKA KWENYE BARABARA,ITAKUWA WAZI KUANZIA TAREHE 1/4/2022. KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA **SIMU NAMBA**
**0716 375 260 AU 0655 611 872.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**DODOMA CHRISTIAN MEDICAL CENTER TRUST** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya Pikipiki aina ya **HONDA CT110** yenye namba za usajili **MC 173 BPC. Chassis NO. JD015309499, Engine NO. JDE2426017.** yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Taarifa ya Polisi.
DOD/DOD/RB/27960/2022.

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**RUKAIYA JUMA ATHUMANI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 873 AYJ , Engine namba dy156d6034741 Chassis namba DY 1256 DY156 FMI 11-124201305 . Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi**
ARU/ARU/RB/52379/2022

## KUPOTEA KWA CHETI



**MENEJA SAITABAU SAITORE**
Anatangaza kupotelewa na cheti cha Kidato cha nne chenye index namba S.11200079 kilichotolewa na Baraza la mitihani kupitia shule ya Sekondari ya **MOITA BWAWANI** mwaka 2018Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa polisi: KIL/MOS/RB/51911/2022**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA IN THE DISTRICT COURT OF ARUSHA
AT ARUSHA
MATRIMONIAL/CASE/ NO 15....2021
EPHRAHIM DANIEL MSANGI.... PLAINTIFF /APPLICATION/D/HOLDER
VERSUS
CATHERINE EPHRAHIM....... DEFENDANT/RESPONDENT /J/DEBTOR
NITICE OF HEARING/MENTION
TO CATHERINE EPHRAHIM**

**TAKE NOTICE** that above case has been fixed for mention/hearing in the District Magistrate's Court of Arusha at Arusha on the **21st day of February 2022 at 08:30am** O'clock in the forenoon.

You may appeal in person or by Advocate or agent duly authorized to appeal on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**TAKE FURTHER NOTICE** That in default of your appearance on that day time before mention or hearing the Court may proceed in your absence .
**GIVEN** under my hard and the seal of the Court this **1st day of February 2022.**

**DISTRICT MAGISTRATE I/C
ARUSHA**
DISTRICT MAGISTRATE I/C
ARUSHA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

METHOD MUSA MSINGWA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T.224 DUK.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI MBE/MBE/RB/53461/2022

## KUPOTEA KWA CHETI



**GERARD THOMAS NGIICHI** anatangaza kupotelewa na cheti cha Kidato cha nne chenye index namba S.121/016 kilichotolewa na Baraza la mitihani kupitia shule ya Sekondari ya
**ST. JAMES SEMINARY** mwaka 1991. Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa polisi: DAR/URA/RB/53027/2022

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## CCM yamwagiza DC kuzuia uchimbaji madini misituni

**Na Idda Mushi, KILOSA**

MKUU wa Wilaya ya Kilosa, Majid Mwanga, ametakiwa kusitisha mara moja shughuli za uchimbaji wa madini kijiji cha Chabima, Kata ya Masanze, kuruhusu maeneo yaliyotengwa kwa shughuli za misitu yasibadilishwe matumizi kiholela na kuwaathiri wananchi.

Maagizo hayo yalitolewa na Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), wilayani Kilosa na Katibu wa Wilaya hiyo, Shaban Mdoe, walipotembelea kijiji hicho kukagua miradi ya maendeleo, ukiwamo wa mkaa endelevu unaotekelezwa na Shirika la Uhifadhi wa Misitu Asilia Tanzania (TFCG) na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA).

Mdoe alisema agizo hilo, limetolewa baada ya kupokea taarifa kutoka kwa wananchi juu ya ujio wa kampuni ya Afrasia Tanzania, inayotaka kuchimba madini katika kijiji hicho, kwenye maeneo yaliyotengwa na kijiji kama hifadhi ya misitu.

"Mkuu wa Wilaya kama msimamizi mkuu wa wilaya, aingilie kati kwani anafahamu taratibu za kubadilisha matumizi kwenye maeneo. Baada ya kubaini kampuni hiyo kufika kijijini kutaka kufanya shughuli ya uchimbaji madini wakiwa na barua ya utambulisho kutoka ofisi ya madini Mkoa, Ofisi ya Mkurugenzi na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS)," alisema Mdoe.

Mdoe alibainisha kwamba ni vigumu kwa eneo moja kuwa na matumizi ya aina mbili, bila kuwa na utaratibu maalum kufuatwa ikiwamo kubadilisha matumizi ya ardhi.

"Kinachoonekana ni kuwa wananchi walidanganywa, Mkuu wa Wilaya lazima uingilie kati na ukishajiridhisha kinachoendelea utufahamishe, kwa sababu wewe ndio unajua taratibu zote za kubadilisha matumizi ya maeneo kwenye wilaya yako," alisema Mdoe.

Mkuu huyo akijibu suala hilo, aliahidi kufanyia kazi na kuonya iwapo watu kulipwa ili kupitisha uchimbaji wa madini, ndani ya hifadhi ya msitu huo akisema ni vyema wakarudisha mapema fedha hizo, kabla ya kuchukuliwa hatua za kisheria.

Katibu wa Kamati ya Maliasili, Iddi Tangula, alisema msitu huo umehifadhiwa kisheria na umekuwa ukiwapatia faida mbalimbali wananchi ikiwa ni pamoja na kujenga zahanati, vyumba vya madarasa katika shule ya msingi na sekondari.

Tangula alisema licha ya mafanikio hayo, bado kumekuwapo na changamoto mbalimbali ikiwamo baadhi yao kutaka kuchimba madini ndani ya msitu ambao umehifadhiwa kisheria.

"Mwenyekiti wa Kijiji hiki, alipeleka maelekezo kwa kamati ya maliasili ya kijiji kuwa, kunatakiwa kutolewa eneo ndani ya msitu kwa ajili ya uchimbaji wa madini na kwamba hayo yalikuwa ni maelekezo kutoka ngazi ya juu," alisema Tangula.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Chabima, Julius Magungu, alisema kampuni hiyo ilifika kijijini hapo na leseni za utafiti kutoka ofisi ya madini ya mkoa, wakiambatana na maofisa mazingira wa halmashauri ya wilaya, kisha kwenda kuangalia eneo walilodai kugundua lina madini na kuanza utaratibu wa kutafuta leseni ya uchimbaji.

# Serikali yapewa kongole kwa marekebisho sheria

**Na Salome Kitomari**

WABUNGE wameipongeza serikali kwa kufanya marekebisho ya sheria iliyozuia kukamatwa tena kwa mtuhumiwa aliyeachiwa kufuatia uamuzi wa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), kuondoa nia ya kuendelea na mashtaka.

Pia wamepongeza kuondolewa kwa kifungu kwenye Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kinachotoa kinga ya kutoshtakiwa kwa polisi wanaofanya operesheni za kificho.

Mbunge wa Viti Maalum, Salome Makamba, alisema: "Kwa kuondoa kifungu cha DPP Taifa linakwenda kupata ahueni kubwa, vijana wengi wasio mrengo na serikali wanasota gerezani baada ya muda mrefu wanaambiwa hakuna kesi, hasa baada ya uchaguzi wanakamatwa mshindi ameshatangazwa ndiyo anaambiwa hakuna kesi."

Alisema wengi waliachiwa kwa kuwa upelelezi haujakamilika au kuna makosa yalifanyika wakati wa kufungua kesi husika, lakini kwa marekebisho hayo kunakwenda kulisaidia taifa.

Mbunge wa Arumeru Magharibi (CCM), Noha Ole Saputu, alisema kutokana na watuhumiwa kuachiwa na kukamatwa tena kulishusha heshima ya mahakama mbele ya umma.

"Ilifika mahali mtu akiachiwa na mahakama anabaki kizimbani kwa sababu alijua akitoka anakamatwa tena. Mabadiliko haya ni mwarobani kwa sasa. Kenya DPP anapomwachia mtu anaeleza sababu kwa uwazi tofauti na hali ilivyokuwa kwetu," alisema.

Aidha, alisema marekebisho hayo yatasaidia kupunguza msongamano wa wafungwa wanaoteseka wengi wakiwa ni wasio na uwezo, huku serikali ikipunguza gharama.

Mbunge wa Kiteto (CCM), Edward Ole Kaita, alisema: "Kama kuna wakati tunawasikia wadau waliotoa maoni yao wakishangilia ni wakati huu kwa kuwa maoni yao yamesikilizwa kwenye muswada huu, imetesa watu wengi wanakaa miaka saba hadi nane, kesi inafutwa inaanza upya sasa inaweka pumziko, madaraka yasitumike vibaya."

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Najma Murtaza Giga, akiwasilisha mapendekezo ya kamati alisema: "Kamati inapongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kuleta mabadiliko haya ya kihitosria kwasababu yana mchango katika maboresho ya mfumo wa uendeshaji wa mashauri ya jinai."

Alisema marekebisho hayo yanaweza kuchangia kurejesha imani ya watuhumiwa kwa mhimili wa mahakama, kwa kuwa hapo awali mtuhumiwa alikuwa haelewi inakuwaje mahakama inamwachia huru na baadaye kukamatwa tena kwa kosa hilo hilo.



Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Kupambana na Vitendo vya Ukatili kwa Watoto na Wanawake (Himiza Development Organization), Prisca Ng'weshemi, akielezea jukumu la shirika hilo lenye maskani yake Kata ya Kitunda, jijini Dar es Salaam katika mkutano maalum mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Sabaya: Video za CCTV zilizoletwa si halisi

**Na Allan Isack, ARUSHA**

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, amedai mahakamani kwamba video za CCTV zilizotoletwa mahakamani kama ushahidi dhidi ya kesi yake si halisi kwa kuwa ziliingizwa kwenye mifumo miwili tofauti.

Pia amedai kwamba vyombo vya dola havikujishughulisha kufanya uchunguzi katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili bali kilichofanyika ni kumbambikia mashtaka.

Sabaya ambaye ni shahidi wa pili kwa mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27 na wenzake sita, alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Patricia Kisinda, wakati akikamilisha kutoa ushahidi wake. Akiulizwa maswali ya nyongeza na Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, Sabaya alidai kwamba katika shauri hilo hakuna uchunguzi uliofanyika na vyombo vya dola na kilichofanyika ni kumbambikia kesi.

Alisema endapo vyombo vya dola vingefanya uchunguzi vingegundua kwamba mashtaka yanayonikabili si ya kweli, bali ni ya kutunga.

Sabaya alisema: "Kama walifanya uchunguzi wangegundua hata gari langu nilinunuaje, kwa kuwa mimi nilikuwa na vyanzo vya mapato, hivyo kwa muktadha huo haki haikutendeka na kama ingetendeka wangehoji na wasingekuja gerezani kutaka kunihoji kwa lazima na kuwataka watu kunibambikia kesi."

Aliieleza kwamba video hizo zinawaonyesha vijana ambao wanadaiwa kuwa ni wa Sabaya wakichukua na kupokea fedha Sh. milioni 90 katika Benki ya CRDB Tawi la kwa Murombo jijini Arusha.

"Shahidi wa saba wa mashtaka aliieleza mahakama kwamba kuna vitu kutoka kwenye mfumo viliongezwa hivyo video hizo, zilizoletwa mahakamani si halisi kwa kuwa kuna baadhi ya vitu viliongezwa kutoka kwenye mfumo mwingine wakati wa uchukuaji," alidai Sabaya.

Aliieleza mahakama hiyo kwamba shahidi mmoja kwa mujibu wa sheria ushahidi wa shahidi mmoja hauwezi kuthibitisha mashtaka yanayowakabili.

Alidai mahakamani kwamba alipekuliwa usiku wa manane na mali zilichukuliwa bila ya kupewa nyaraka.

"Sheria inataka mtu kupekuliwa kwa nyaraka na anayefanya kunyume na sheria hana tofauti na jambazi na atakuwa amevunja sheria kwa mantiki ya kutafuta haki," alidai Sabaya na kuongeza:

"TAKUKURU walichukua mali zangu na mali za watu wengine bila kufuata utaratibu na walichukua gari langu bila kutoa risiti na kwa mantiki hiyo wanavunja sheria kwa makusudi."

Pia alidai mahakamani huko kwamba hakumwagiza mfanyabiashara Francis Mroso kutoa Sh. milioni 90.

Katika hatua nyingine, baada ya Sabaya kukamilisha kutoa ushahidi wake, Wakili Mahuna, aliiomba mahakama hiyo, kuahirisha usikilizwaji wa shauri hilo hadi Februari 16, mwaka huu, kwa kuwa wana kesi nyingine katika Mahakama ya Rufani Februari 08, 14 na 15.

# PRISONS YAKIMBIA NELSON MANDELA, YARUDI SOKOINE

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Tanzania Prisons imeamua kurejesha mechi zake za nyumbani katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya kuanzia hatua iliyobaki msimu huu.

Tangu ihamie Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga mkoani Rukwa, Prisons imekuwa na mwenendo mbaya katika Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa pili mfululizo sasa.

Kwa sasa Tanzania Prisons inashika mkia kwenye Ligi Kuu, ikiwa imeambulia pointi 11 tu katika mechi 14 ilizocheza hadi sasa.

Katika taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari juzi kupitia idara ya mawasiliano ya klabu hiyo, ilieleza: "Tunapenda kuwafahamisha kuwa timu ya Tanzania Prisons Sports Club kwa sasa itatumia Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya kama uwanja wake wa nyumbani katika michezo yake yote ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara na mashindano yote yatakayoihusu timu."

Imesema awali ilikuwa ikitumia Uwanja wa Nelseon Mandela ili kupisha marekebisho ya uwanja wao wa mazoezi sambamba na makazi ya wachezaji pamoja na viongozi ambayo kwa sasa yamekamilika.

"Tunaushukuru uongozi mzima wa mkoa wa Rukwa kupitia ofisi ya mkuu wa mkoa, viongozi wa chama cha mpira wa Sumbawanga, wananchi na wadau mbalimbali wa michezo kwa mapokezi na ushirikiano mkubwa mliotupatia kwa kipindi chote ambacho tumekuwa pamoja. Prisons ni ya Tanzania na ipo kwa ajili ya kutoa burudani kwa Watanzania," ilieleza taarifa hiyo.

## NAMNA HII...



Sajenti Juma Makame Mnyaa wa Kikundi cha Sanaa cha Jeshi la Polisi, akionyesha umahiri wa kucheza ngoma ya Kibati wakati wa uzinduzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: Jumanne JUMA**

## Mtibwa: Mechi na Yanga ni Manungu

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mtibwa imesisitiza kuwa mechi yake dhidi ya Yanga inayotarajiwa kuchezwa Februari 23, mwaka huu, itapigwa kwenye Uwanja wa Manungu Complex kama kawaida na hakuna chochote kile ambacho kitawafanya kuihamisha mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Msemaji wa klabu hiyo, Thobias Kifaru, aliyasema hayo juzi kwenye Uwanja wa Ilulu mjini Lindi wakati timu yake ikicheza mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Namungo na kuchakazwa mabao 3-1.

Kifaru alisema Yanga wafikirie kusafiri hadi Manungu na si vinginevyo, kwani hakuna mpango wowote wa kuihamisha mechi hiyo kama ambavyo amekuwa akisikia tetesi hizo.

"Niwahakikishie kuwa mechi yetu dhidi ya Yanga inachezwa kwenye Uwanja wa Manungu Complex na si uwanja mwingine wowote ule. Kwa hiyo niwatake tu wale wa Yanga, wafikirie kusafiri kwenye mashamba ya miwa.

"Kila kitu kwetu kipo sawa, wala wasifikiri tutabadilisha uwanja, nilisifu Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Bodi ya Ligi kwa kuupitisha uwanja wetu kuchezea mechi za ligi, pamoja na timu kubwa ambazo zaidi ya miaka 20 zilikuwa haziji Manungu," alisema Kifaru.

Hivi karibuni zilizuka tetesi kuwa huenda Mtibwa Sugar ikabadilisha uwanja kutoka kwenye Manungu Complex na kupeleka uwanja mwingine, kitu ambacho baadaye klabu ilikanusha, ingawa bado mashabiki wa soka walikuwa na wasiwasi na hilo.

Kwa mara ya kwanza Mtibwa Sugar ilicheza dhidi ya Simba kwenye uwanja huo kwa mara ya kwanza zaidi ya miaka 20, Januari 22 na timu hizo kutoka suluhu.

# 'VAR za Mwigulu' zaibua mapya

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuibuka mjadala mkubwa kuhusu Matumizi ya Teknolojia ya Video ya Kumsaidia Mwamuzi (VAR), kuwekwa kwenye viwanja hapa nchini, Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, naye aibuka na kutoa maoni yake kwa kueleza kwamba kipaumbele kikubwa kinapaswa kuwa kuboreshwa kwa eneo la kuchezea kwanza kwa viwanja kuwekwa nyasi bandia.

Jusi Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kupitia ukurasa wake wa Instagram aliahidi kumtafutia fedha Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa kwenye bajeti ijayo ili kuweka Mashine za VAR kwa ajili ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Waziri Mwigulu alitoa kauli hiyo jana kwa kuandika kupitia mtandao wake wa kijamii na Instagram, huku akiwa ameweka video ndogo ya mechi kati ya Yanga na Mbeya City iliyochezwa juzi usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, wakati timu hizo zikitoka suluhu. Video hiyo fupi ilikuwa ikionyesha straika wa Yanga, Fiston Mayele akiwa anapokea pasi na mwamuzi msaidizi kuonyesha kuwa ameotea, wakati kupitia picha za marudio zikionyesha hakuwa ameotea.

Lakini jana kupitia ukurasa wake wa Instagram, Ahmedy aliandika: "Nimeona mjadala wa VAR, ni wazo zuri naamini nia ni kuufanya mpira wa nchi hii uendelee kuwa bora zaidi.

"Lakini kwangu VAR sio tatizo la msingi la mpira wetu. Tatizo la msingi la mpira wetu ni sehemu ya kuchezea (pitch). Tuna pitch mbovu sana nchi hii ukitoa Taifa, Azam Complex na Kaitaba, viwanja vingi vilivyosalia ni changamoto."

Alisema mpaka leo viwanja vyetu vinapakwa chokaa kabla ya mechi na baada ya muda inafutika uwanja unakua hauna mistari na mvua zikinyesha kidogo tuu mpira hauchezeki.

Alisema mechi nyingi zinachezwa kwa kulazimishwa akitolea mfano mechi ya Mbeya City dhidi ya Ruvu Shooting haikupaswa kuchezwa Uwanja wa Sokoine.

"Ushauri wangu kabla ya 'ku-invest' (kuwekeza) kwenye VAR tungejikita kuboresha viwanja, Europe (Ulaya) walianza kuboresha viwanja ndio wakaja kwenye VAR," alisema.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**RONALDO HAELEWEKI UNITED**
MSHAMBULIAJI wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, atasubiri hadi Manchester United itakapotangaza utambulisho wa kocha wao mpya kabla ya kuamua ikiwa atasalia hapo Old Trafford. ***(ESPN)***

**ARSENAL KUSAJILI NYOTA**
ARSENAL wanapanga kutumia hadi pauni milioni 180 msimu huu wa majira ya joto kumsajili kiungo wa kati wa Wolves na Ureno, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 24, mshambuliaji wa Everton na England, Dominic Calvert-Lewin mwenye miaka 24, pamoja na Alexander Isak (22), kutoka Real Sociedad. ***(Sun)***

**OSIMHEN AWANIWA SPURS**
KLABU ya Tottenham Hotspur inapania kumsajili mshambuliaji wa Napoli, Victor Osimhen katika msimu wa joto baada ya kumkosa Mnigeria huyo mwenye umri wa miaka 23, ambaye alitemwa na klabu hiyo ya Italia katika dirisha la uhamisho wa Januari. ***(Football Insider)***

**ROMA KUMUUZA ZANIOLO**
KLABU ya AS Roma ipo tayari kupokea ofa kiasi cha euro milioni 40 kwa ajili ya mshambuliaji wa Italia, Nicolo Zaniolo, huku Juventus na Tottenham Hotspur zikiwa miongoni mwa klabu zinazomtaka kiungo huyo wa miaka 22. ***(Calciomercato)***

**NDOMBELE KURUDI SPURS**
KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Tanguy Ndombele amesema kazi yake Tottenham Hotspur "haijaisha" baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, kurejea Lyon. ***(RMC Sport via Mirror)***

**SALIBA AWINDWA WEST HAM**
KLABU ya West Ham msimu wa majira ya joto inapanga kumsajili beki wa kati wa Arsenal na Ufaransa, William Saliba mwenye umri wa miaka 20, ambaye yuko Marseille kwa mkopo. ***(Jeunes Footeux via Sport Witness)***

**CARVALHO ANUKIA LIVER**
LIVERPOOL huenda ikafufua nia ya kumsaka Fabio Carvalho msimu wa joto baada ya kukaribia kumsajili mshambuliaji huyo wa Fulham mwezi uliopita. ***(AS - in Spanish)***

**ZIDANE BADO KUAMUA**
KOCHA wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane mwenye umri wa miaka 49, bado hajakubali kuwa mrithi wa Mauricio Pochettino kama kocha wa Paris St-Germain kwa sababu anasubiri kuona ikiwa Didier Deschamps ataachia jukumu lake kama kocha wa Ufaransa. ***(RMC Sport)***

**COSTA AIKATAA FLAMENGO**
WINGA Brazil, Douglas Costa mwenye umri wa miaka 31, amepuuzia mbali ombi la Flamengo na kukubali kujiunga na klabu ya MLS LA Galaxy kwa mkopo wa miezi sita kutoka Juventus. ***(Fabrizio Romano)***

**BOTMAN AWANIWA NEWCASTLE**
KLABU ya Newcastle itafufua nia yake ya kumsajili mlinzi wa Lille, Sven Botman mwenye umri wa miaka 22 ikiwa atapona kushushwa daraja kutoka kwenye Ligi Kuu England. ***(Athletic)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RAIS WA SENEGAL ATANGAZA LIKIZO KUSHEREHEKEA AFCON

Ni baada ya kuifunga Misri mechi ya fainali, Mane naye asema wamengoja ushindi huo kwa miaka 60, hivyo...

**DAKAR, Senegal**

RAIS wa Senegal, Macky Sall alitangaza jana Jumatatu kuwa siku ya mapumziko kusherehekea ushindi wa timu ya taifa baada ya juzi kutwaa Kombe la Mataifa ya Afrika, Afcon.

Rais huyo ambaye alikuwa nje ya nchi, alifutilia mbali awamu ya mwisho ya safari yake ili kuwakaribisha nyota hao wa soka waliorejea Senegal jana Jumatatu.

Rais Sall ataitunuku timu hiyo leo Jumanne katika ikulu ya rais, televisheni ya RTS ilisema.

Senegal ilishinda fainali ya kwanza ya Afcon baada ya kushindwa mara mbili katika fainali mwaka 2002 na 2019.

Waliishinda Misri kwa mikwaju ya penalti 4-2 na kupata ushindi wao baada ya fainali kumalizika bila bao kufuatia muda wa nyongeza.

"Tumengoja ushindi huu kwa miaka 60," alisema Sadio Mane ambaye alifunga penalti ya ushindi na kuipa Senegal taji la kwanza la Afcon. Mechi hiyo ya fainali ilichezwa kwenye Uwanja wa Olembe jijini Yaounde nchini Cameroon ambapo walimaliza dakika 120 bila kufungana na kuamuliwa kwa mikwaju ya penalti.

Mane alikosa penalti katika kipindi cha kwanza kabla ya kuja kusahihisha makosa yake na kufunga penalti ya ushindi kwa taifa lake na kuipa Senegal ubingwa huo kwa mara ya kwanza katika historia yao.

Kipa wa Chelsea, Edouard Mendy alikuwa shujaa wa Senegal, akiokoa penalti ya mchezaji wa akiba Mohanad Lasheen kabla ya Mane kufunga penalti yake ya ushindi.

Hii ni mara ya kwanza kwa Simba hao wa milima ya Teranga kutwaa ubingwa wa Afcon baada ya kucheza jumla ya fainali tatu wakiwa wamecheza mashindano hayo mara 16.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT
TZS. 918

MECHI KALI
BURNLEY
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 5.30
X | 3.89
2 | 1.63

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# RANGNICK MAMBO MAGUMU UNITED

**MANCHESTER, England**

WACHEZAJI wa klabu ya Manchester United hawajafurahishwa na kocha wa muda, Ralf Rangnick, huku Mjerumani huyo akiendelea kuwa katika wakati mgumu na wachezaji wake.

Akiwa amewasili kuchukua nafasi ya Ole Gunnar Solskjaer mwishoni mwa mwaka 2021, Rangnick alitarajiwa kuleta mapinduzi pale Old Trafford.

Lakini, badala yake, amekuwa akitengeneza vichwa vya habari mara kwa mara kwa kuwakera wachezaji wake.

Baada ya kutolewa kwenye Kombe la FA dhidi ya Middlesbrough Ijumaa, iliibuka kuwa kikosi cha United hakina furaha na kocha wao, ingawa si kwa sababu ya kushindwa.

Kwa mujibu wa gazeti la The Sun, bosi huyo anakabiliwa na mzozo mkali kutoka kwa wachezaji wake baada ya kusema hadharani kuwa Jesse Lingard aliomba asicheze kabla ya mchezaji huyo kuibuka na kusema si kweli kabisa, badala yake akasema klabu ndiyo imemshauri kuchukua mapumziko.

"Ni wakati wa kuwa pamoja, si kusababisha mgawanyiko kwa kuzungumza hadharani," chanzo cha ndani kiliripotiwa kuliambia The Sun.

"Si njia ya kufanya mambo United, kwenda nje na kutangaza masuala haya kwenye vyombo vya habari."

# Uefa yapinga wazo la Fifa

**NYON, Uswisi**

RAIS wa Shirikisho la Soka la Ulaya (UEFA), Aleksander Ceferin, amepinga wazo la Kombe la Dunia kuchezwa kila baada ya miaka miwili na amependekeza kuwa na kikao cha wazi kwa viongozi watatu waasisi wa Super league.

Rais wa Shirikisho la Soka la Duniani (FIFA), Gianni Infantino anajaribu kushawishi michuano ya Kombe la Dunia ichezwe kila baada ya miaka miwili, kitu ambacho kinapingwa na idadi kubwa ya washikadau wa mchezo wa mpira wa miguu, kwa kuogopa kuondoa ladha na historia.

UEFA hivi karibuni wameanzisha michuano mipya ya ligi ya timu za taifa ambapo mashindano hayo yanaenda sambamba na ligi za klabu ambazo zinachezwa kila baada ya miaka miwili.

Ceferin alinukuliwa akiwa kwenye mahojiano na Journal du dimanche akisema, "nina uhakika Kombe la Dunia halitachezwa kila baada ya miaka miwili, kwa sababu ni wazo la kijinga."

"Inaonekana kwangu kuwa shirikisho la mpira lingekuja na wazo la kupunguza kalenda ambayo wachezaji wanaangaika nayo.

"Tuna miezi mimgi ya kucheza kila majira ya joto, Kombe la Dunia, Kombe la Shirikisho na mashindano mengine mengi, miongoni mwa haya yataharibu mpira wa wanawake," alisema Ceferin.



## HABARI MICHEZO


,137,180

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 12/02/21 | 18:00 | Brentford vs Crystal Palace | 2.60 | 3.09 | 2.84 |
| 02. 12/02/21 | 18:00 | Peterborough vs Preston | 2.75 | 3.15 | 2.51 |
| 03. 12/02/21 | 18:00 | Reading vs Coventry | 2.79 | 3.19 | 2.45 |
| 04. 12/02/21 | 18:00 | Birmingham vs Luton Town | 2.81 | 3.15 | 2.46 |
| 05. 12/02/21 | 18:00 | Nottingham vs Stoke City | 2.31 | 3.14 | 3.04 |
| 06. 12/02/21 | 18:15 | Villarreal vs Real Madrid | 2.74 | 3.32 | 2.54 |
| 07. 12/02/216 | 18:15 | Perugia vs Frosinone | 2.40 | 3.14 | 2.90 |
| 08. 12/02/21 | 20:00 | Napoli vs Inter | 2.81 | 3.41 | 2.44 |
| 09. 13/02/21 | 15:00 | Sheffield Wed vs Rotherham | 2.79 | 3.13 | 2.49 |
| 10. 13/02/21 | 16:00 | Alaves vs Valencia | 3.04 | 3.24 | 2.36 |
| 11. 13/02/21 | 18:00 | Real Oviedo vs Huesca | 2.46 | 3.15 | 2.81 |
| 12. 13/02/21 | 19:00 | Kasimpasa vs Alanyaspor | 2.61 | 3.30 | 2.56 |
| 13. 13/02/21 | 19:30 | Leicester vs West Ham | 2.85 | 3.45 | 2.38 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 08/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2936 | Honka vs Haka | 2.32 | 3.20 | 3.20 |
| 14:30 | 3126 | Kasimpasa vs Gaziantep BB | 2.06 | 3.33 | 3.18 |
| 15:40 | 4556 | Alshoulla vs Najran SC | 1.80 | 3.18 | 4.34 |
| 16:00 | 1047 | Busoga United vs Mbarara FC | 5.00 | 3.08 | 1.74 |
| 16:00 | 2749 | Sabah vs Gabala | 2.35 | 3.04 | 2.89 |
| 16:00 | 2784 | Watford U23 vs Colchester U23 | 2.12 | 3.80 | 2.74 |
| 16:00 | 3879 | Tooro United vs Onduparaka FC | 4.04 | 3.27 | 1.83 |
| 16:00 | 4133 | Sepsi Osk vs Gaz Metan Medias | 1.52 | 3.68 | 6.67 |
| 16:00 | 5369 | Cardiff City U23 vs QPR U23 | 1.44 | 4.65 | 5.23 |
| 16:30 | 1438 | Millwall U23 vs Ipswich U23 | 2.41 | 3.51 | 2.50 |
| 17:00 | 5431 | Hyderabad FC vs ATK Mohun Bagan | 2.21 | 3.32 | 2.89 |
| 17:30 | 4825 | Fatih Karagumruk vs Konyaspor | 2.36 | 3.22 | 2.74 |
| 18:15 | 3525 | Sabayil vs FK Sumgayit | 3.09 | 2.65 | 2.51 |
| 18:30 | 4804 | CFR Cluj vs UTA Arad | 1.40 | 3.92 | 9.01 |
| 18:55 | 5702 | Al Wehda vs AL Jeel | 1.64 | 3.65 | 5.80 |
| 19:30 | 5638 | Palmeiras vs Al Ahly Cairo | 1.46 | 3.94 | 6.16 |
| 20:30 | 1707 | Fenerbahce vs Kayserispor | 1.45 | 4.34 | 5.60 |
| 20:30 | 3655 | Karlsruher SC vs Sandhausen | 2.00 | 3.48 | 3.43 |
| 20:55 | 2225 | Voluntari vs Rapid Bucuresti | 2.28 | 3.05 | 3.19 |
| 21:00 | 2306 | PSV Eindhoven vs NAC Breda | 1.05 | 9.69 | 24.23 |
| 21:00 | 3679 | CD Feirense vs Sporting Farense | 2.25 | 3.23 | 3.03 |
| 22:00 | 1249 | Yverdon-Sport FC vs Lausanne-Sport | 2.90 | 3.43 | 2.16 |
| 22:45 | 1307 | Linfield Belfast vs Larne | 1.89 | 3.43 | 3.57 |
| 22:45 | 1384 | Newcastle vs Everton | 2.50 | 3.36 | 2.76 |
| 22:45 | 1647 | Carrick Rangers vs Cliftonville Belfast | 5.20 | 4.05 | 1.51 |
| 22:45 | 1892 | Luton Town vs Barnsley | 1.60 | 3.68 | 5.49 |
| 22:45 | 1964 | Derby vs Hull City | 2.31 | 3.09 | 3.09 |
| 22:45 | 2165 | Fleetwood Town vs MK Dons | 3.04 | 3.23 | 2.26 |
| 22:45 | 2229 | Crusaders Belfast vs Ballymena Utd | 1.50 | 4.05 | 5.41 |
| 22:45 | 2381 | Stoke City vs Swansea | 2.21 | 3.19 | 3.19 |
| 22:45 | 2403 | Portsmouth vs Burton | 1.93 | 3.39 | 3.73 |
| 22:45 | 2726 | Coleraine FC vs Dungannon Swifts | 1.46 | 4.25 | 5.60 |
| 22:45 | 2869 | Lincoln vs Morecambe | 1.73 | 3.58 | 4.51 |
| 22:45 | 2880 | Wycombe vs Shrewsbury | 1.92 | 3.44 | 3.74 |
| 22:45 | 3060 | Doncaster vs Ipswich | 4.10 | 3.57 | 1.80 |
| 22:45 | 3170 | Accrington vs Oxford Utd | 2.84 | 3.24 | 2.38 |
| 22:45 | 3712 | Cheltenham vs Sunderland | 3.34 | 3.39 | 2.06 |
| 22:45 | 4169 | Fulham vs Millwall | 1.32 | 4.91 | 8.24 |
| 22:45 | 4417 | Sheffield Wed vs Wigan | 2.27 | 3.23 | 3.03 |
| 22:45 | 4437 | Coventry vs Blackpool | 1.87 | 3.38 | 4.01 |
| 22:45 | 4738 | West Ham vs Watford | 1.42 | 4.80 | 6.80 |
| 22:45 | 4986 | Gillingham vs Cambridge Utd | 2.90 | 3.19 | 2.37 |
| 22:45 | 5168 | AFC Wimbledon vs Rotherham | 5.13 | 3.85 | 1.60 |
| 22:45 | 5452 | Crewe vs Plymouth | 3.34 | 3.34 | 2.08 |
| 22:45 | 5941 | Portadown FC vs Glentoran Belfast | 6.16 | 4.43 | 1.41 |
| 23:00 | 2929 | Bolton vs Charlton | 2.24 | 3.28 | 3.04 |
| 23:00 | 5309 | Burnley vs Manchester Utd | 5.30 | 3.89 | 1.63 |
| 23:00 | 5365 | Inter vs Roma | 1.57 | 4.25 | 4.94 |
| 23:00 | 5749 | Monaco vs Amiens | 1.33 | 4.82 | 8.66 |
| 23:15 | 3308 | CF Estrela vs Academica | 1.86 | 3.46 | 3.85 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# JOB AMWOMBA RADHI MCHEZAJI MBEYA CITY

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa Yanga, Dickson Job, amemwomba radhi mchezaji Richardson Ng'ondya wa Mbeya City kutokana na rafu aliyomfanyika kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na timu hizo kutoka suluhu.

Job ameomba radhi kwenye mtandao wake wa Instagram, baada ya rafu aliyoifanya kwenye mechi hiyo kwa kumkanyaga Ng'ondya akiwa ameanguka chini, kitu ambacho kilisababisha mjadala mkali kwenye mtandao wa kijamii, huku video yake fupi ikisambaa katika mitandao mbalimbali.

"Mimi kama mchezaji nina wajibu wa kulinda afya yangu na ya mchezaji mwenzangu. Nimechukua hatua za kuwasiliana na Richardson Ng'ondya wa Mbeya City na kumjulia hali kutokana na ajali iliyotokea kwenye mchezo huo na kamwe sijawahi kuwa na dhamira ya kuhatarisha afya ya mchezaji mwenzangu, lakini ajali hutokea michezoni. Nachukua nafasi hii kuomba radhi kwa wote waliosumbuliwa na ajali ile na naahidi kuwa makini zaidi wakati ujao," aliandika mchezaji huyo.

Tukio hilo linakuja wakati beki mwingine wa klabu hiyo, Djuma Shaaban akitumikia adhabu ya kukosa mechi tatu baada ya kufungiwa na Bodi ya Ligi kutokana na kumpiga kiwiko mchezaji wa Polisi Tanzania, Yahaya Mbegu kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa Januari 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha, Yanga ikishinda bao 1-0.




Dickson Job

# Biashara yaiwinda Yanga SC Magomeni

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Biashara United, kimeweka kambi Magomeni jijini Dar es Salaam kwa ajili ya maandalizi ya mchezo wa hatua ya 16-bora ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC), maarufu FA Cup dhidi ya Yanga.

Biashara United itakuwa ugenini dhidi ya Yanga mchezo utakaopigwa Februari 15, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Biashara United, Vivier Bahati, alisema baada ya kumalizika mchezo wao dhidi ya KMC FC wa Ligi Kuu Tanzania Bara, hawakutaka kurejea Musoma na badala yake wameendelea kubaki Dar es Salaam kwa maandalizi ya mechi hiyo ya Kombe la FA.

Alisema lengo kubwa la kubaki Dar es Salaam ni kufanya maandalizi kuelekea mchezo wa hatua ya 16-bora dhidi ya Yanga ili kuhakikisha wanafanya vizuri kwa kupata matokeo chanya na hatimaye kusonga mbele.

"Tuko jijini Dar es Salaam hatujaondoka, tumebaki kwa ajili ya kufanya mazoezi ya kujiandaa na mchezo wa Kombe la Shirikisho dhidi ya Yanga," alisema Vivier.

Alisema anafanyia kazi madhaifu yaliyojitokeza katika mechi zilizopita ikiwamo safu ya ushambuliaji kwa kuwa mechi dhidi ya KMC FC walitengeneza nafasi nyingi na kushindwa kuzitumia.

Michezo

Jumanne Februari 8, 2022

Nipashe



## Rais wa Senegal atangaza likizo kusherehekea Afcon

KWISHINE...




Kiungo wa Simba, Clatous Chama akishangilia baada ya kuifungia timu yake bao pekee wakati ikiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Mbeya Kwanza kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. Kulia ni Hassan Dilunga na kushoto ni Sadio Kanoute. **PICHA: simba**

# SIMBA YATAJA SABABU KUKOSA MABAO LIGI KUU

●●●Yarudi kambini kutafuta dawa ikiisubiri Asec Mimosas michuano CAF Jumapili...

**Na Waandishi Wetu**

BAADA ya kupata ushindi kwa shida nyumbani katika mechi mbili mfululizo, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola ameweka wazi kuwa wanapata ugumu kwa timu ambazo zinaamua kukaa nyuma maarufu kama 'kupaki basi', huku akikiri pia ubutu wa safu ya ushambuliaji wa timu hiyo kwa sasa.

Simba juzi iliibuka na ushindi finyu wa bao 1-0 tena kwa tabu katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Mbeya Kwanza, mchezo huo ukiwa ni baada ya kupata ushindi kama huo kwa penalti kwenye mechi iliyopita dhidi ya Tanzania Prisons.

Akizungumza kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa baada ya kumalizika kwa mechi dhidi ya Mbeya Kwanza juzi, Matola alisema wapinzani wao waliiga mfumo kama wa Prisons kucheza kwa 'kupaki basi', hivyo ikawapa ngumu kwao kuwafungua.

Pamoja na hayo, Matola amekiri kuwapo kwa ubutu kwenye safu ya ushambuliaji wa timu hiyo, lakini akaongeza kuwa hao ndiyo washambuliaji waliokuwa nao kwa sasa na msimu uliopita na mingine waliwapa mafanikio makubwa.

"Tulikuwa wazuri vipindi vyote viwili, Mbeya Kwanza wao walikuja kwa kuiga mfumo wa Prisons wa kukaa nyuma, lakini pamoja na hayo tungekuwa makini kipindi cha kwanza tungeweza kupata hata mabao mawili, tulipoteza nafasi za wazi za kufunga, kipindi cha pili wakaendelea na mfumo wao kwa sababu bado ulikuwa unafanya kazi vizuri, lakini tukaitumia nafasi moja tuliyoipata," alisema Matola.

Alibainisha kuwa inakuwa tabu sana kwao kuifungua timu ambayo 'inapaki basi', jambo ambalo sasa wataenda kulifanyia kazi.

"Walituheshimu, wakarudi nyuma wote na ilikuwa ngumu sana kwetu kuwafungua kwa sababu hata mipira mirefu tukipiga inakuwa haina umuhimu kwetu, kipa wao anaiwahi, tulichoamua ni pasi tu fupi fupi, ambazo nazo wakati mwingine zilishindwa kupita kutokana na kuwa wengi golini wakiwa karibu na kipa wao, ila tunashukuru tumepata nafasi hiyo, tutaendelea kuangalia ni jinsi gani ya kucheza na timu za aina hiyo," alisema kocha huyo ambaye ni mechi yake ya mwisho kusimamia timu, kwani Kocha Mkuu Pablo Franco amemaliza adhabu yake ya kufungiwa mechi tatu.

Aidha, alisema wamerudi mazoezini kujiandaa na mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Asec Mimosas utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili wiki hii.

"Mechi inayofuata ni Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya ASEC Mimosas, tuna muda wa siku sita kuwaandaa wachezaji wetu kisaikolojia na mazoezi ili tupate ushindi nyumbani. Huu ni mchezo mkubwa na muhimu sana kuhakikisha tupambana na kutafuta ushindi tukiwa nyumbani," alisema Matola.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Mbeya Kwanza, Maka Mwalwisi, amesema ilikuwa mechi nzuri, kila timu ikiingia kwenye mpango kazi wake na waliweza kuizuia Simba kwa dakika 79.

***Imeandaliwa na Saada Akida, Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo***

## GSM yajitoa udhamini Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

KAMPUNI ya GSM imetangaza rasmi kujitoa kwenye nafasi ya mdhamini mwenza wa Ligi Kuu Tanzania Bara inayodhaminiwa na Mdhamini Mkuu Benki ya NBC.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Ofisa Biashara Mkuu wa Kampuni hiyo, Allan Chonjo, amesema pamoja na sababu nyingine, lakini kubwa iliyofanya kufikia maamuzi hayo ni kuwa Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Bodi ya Ligi kushindwa kutekeleza baadhi ya vipengele vya mkataba kama ambavyo pande mbili zilivyokubaliana awali.

Mbali na hilo, Ofisa Biashara Mkuu huyo kwa niaba ya Ghalib Said Mohamed ambaye ni Mwenyekiti na Mjumbe wa Kamati ya Ushindi ya Taifa Stars, ametangaza kuwa kiongozi huyo amejiuzulu kwenye nafasi hizo zote mbili katika kamati hiyo.

"Leo tarehe 7, Februari 2022, uongozi wa GSM unatangaza rasmi kujiondoa kwenye nafasi ya kuwa Mdhamini Mwenza wa Ligi Kuu ya NBC na sababu kubwa iliyofanya hata kufikia maamuzi haya ni kwa TFF na Bodi ya Ligi kushindwa kutekeleza baadhi ya vipengele vya kimkataba kama pande zote mbili zilivyokubaliana.

"Ikumbukwe kuwa GSM ilishawishika sana na TFF pamoja na Bodi ya Ligi na kuridhia kuwa mdhamini mwenza wa Ligi Kuu ili kukuza sekta hii ya mpira wa miguu hapa nchini pamoja na michezo kwa ujumla, lakini hii haikuenda kama ilivyokusudiwa," alisema ofisa huyo wakati akitangaza uamuzi huo.

Kuhusu Ghalib kujitoa kwenye Uenyekiti na Kamati ya Stars, alisema kuwa ameamua kufanya maamuzi hayo magumu ya kujiuzulu, lakini anawashukuru viongozi wote katika nafasi mbalimbali.

Kampuni hiyo iliingia udhamini huo mwezi Novemba mwaka jana, klabu 15 zikiafiki, kasoro Klabu ya Simba tu ambayo ilipinga udhamini huo, lakini suala hilo lilifikishwa Tume ya Ushindani (FCC), likitakiwa kuchunguzwa na kutolewa uamuzi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >